SUPA JACKPOT
TZS. 1,154,861,566
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Muhimbili** mara ya kwanza yafanya upasuaji wa kifua kwa tundu dogo

UKURASA 3




UKURASA 11

Nipashe
Jumatano Septemba 20, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581439
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Rais ang'aka kuletewa madai yenye miaka 20

• **Ahoji** waliko viongozi, mbunge kulinyamazia... *Uk.2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**RAIA WA MAREKANI KORTINI KUJIPATIA KITAMBULISHO CHA NIDA**

RAIA wa Marekani, Yaki Juma, amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam...

UKURASA WA 8

**MTAALAMU AONYA WATOTO KUFUNGIWA NYUMBANI**

MTAALAMU wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, Davis Gisuka, ameonya wazazi wenye tabia ya...

UKURASA WA 14



SALIM AHMED SALIM: **ALITIKISA USHINDANI KATIBU MKUU UN, ALIANZA UBALOZI NA MIAKA 22**



Rais Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliyetoa ufafanuzi kuhusu vifaa vya kisasa vya uvuvi, baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Kilwa Masoko, mkoani Lindi jana. **PICHA: IKULU**

## Dk. Anna Henga: Hiki kinanifurahisha kwa Rais Dk. Samia

UKURASA 4




Mpigakura akisaidiwa kuingia katika kituo cha kupiga kura ili kutimiza haki yake ya kumchagua kiongozi anayemtaka katika uchaguzi wa diwani wa Kata ya Mfaranyaki, kwenye kituo cha Ofisi ya Kata namba 2 Halmashauri ya Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Umeme kwa ratiba waanza rasmi

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA YAREJEA KWENYE SHOO ZAKE ZA 5G UK.24 **KATUNI** UK.6



Mkuu mteule wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa (kulia), akisalimiana na Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara, Kheri James, baada ya kuweka jiwe la msingi la jengo la kitega uchumi la KKKT Dayosisi ya Mbulu, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Rais ang'aka kuletewa madai yenye miaka 20

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema inashangaza anapoombwa kushughulikia matatizo ya wananchi ya miaka 20 iliyopita ilhali walikuwapo viongozi waliopaswa kuyashughulikia.

Samia alisema hayo jana baada ya Mbunge wa Kilwa Kusini, Ally Kasinge, kumwomba aweke msukumo ili wananchi 438 wa Kilwa Masoko waliopisha ujenzi wa uwanja wa ndege tangu mwaka 2013 walipwe fidia zao.

Rais pia alikemea baadhi ya viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa wanaotumia fedha za miradi ya maendeleo kwa manufaa binafsi na kuwataka wajitathmini kama fedha zinatololewa na serikali hazitabadilisha halmashauri hiyo kiuchumi.

Alisema hayo katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa bandari ya uvuvi na ugawaji wa boti za kisasa kwa wavuvi wa Kilwa Masoko, wilayani Kilwa ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake mkoani Lindi.

Katika ziara hiyo, Rais pia aliweka mawe ya msingi katika Shule ya Wasichana ya Lindi iliyoko kijiji cha Kilangala, Wilaya ya Lindi na Hospitali ya Rufani ya Mkoa katika kijiji cha Mitwero wilayani Lindi.

Alisema wakati anaingia bungeni mwaka 2010, aliyekuwa Mbunge wa Kilwa Kusini, Suleiman Buranga, maarufu kama Bwege, alikuwa akiyazungumzia madai hayo lakini anashangaa mpaka sasa hayajalipwa.

"Miaka 20 yote Kilwa si mlikuwa na viongozi? Si mlikuwa na wabunge wanawawakilisha? Kwa nini madai haya yamekaa muda wote huo bila kushughulikiwa?" Alihoji Rais Samia huku akiwataka viongozi wa halmashauri hiyo kuyaangalia tena kabla ya kumpelekea, ili wachunguze kama kuna kasoro au sababu zilizofanya kutofanyiwa kazi muda wote huo.

Pia alisema amepata taarifa za baadhi ya viongozi wakiwamo madiwani na wenyeviti wa halmashauri kuhusu usimamizi usiofaa wa fedha za miradi ya maendeleo zinazopelekwa katika halmashauri hiyo.

Rais aliwaonya wavuvi wa wilaya hiyo wanaotumia baruti katika shughuli zao kuwa zinachangia kwa kiasi kikubwa kuwapo uhaba wa samaki kwa kuwa wanakimbia kwenye maji mengi kutafuta makazi ambayo yameharibiwa.

Alisema serikali inajitahidi kutoa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika wilaya hiyo, hivyo kama haitabadilika kimaendeleo miaka ijayo, viongozi wanapaswa kujitathmini.

"Niwaambie tu kwamba hizi fedha zinaletwa kwa ajili ya kuondoa dhiki na changamoto za wananchi. Hizi fedha hazijaletwi viongozi mjinufaishe. Ndio maana nasema kwa mtiririko huu wa fedha, Kilwa yetu hii isipobadilika viongozi kaeni mjitizame kuna nini ndani yenu," alisema.

Rais alisema serikali imetoa boti kwa wavuvi na wakulima wa mwani kwa bei nafuu ikitambua hali halisi za vipato vyao na kuwasihi waliopewa zana hizo wazitumie kujiinua kiuchumi na kulipa mikopo ili itumike kununua zingine.

Pia alisema serikali ina mpango wa kujenga bandari nyingine ya uvuvi Bagamoyo ili kukidhi mahitaji ya meli nyingi zinazotarajiwa kuingia nchini kufuata fursa za uvuvi.

Kuhusu ombi lililotolewa na Kasinge kufuta hati ya eneo la mwekezaji wa Kilwa Yatch Club, Pwani ya Jimbiza, Rais alisema uamuzi huo utasababisha serikali kuilipa fedha nyingi kampuni hiyo iwapo itafungua kesi mahakamani, hivyo kuwaathiri wavuvi wanaotumia eneo hilo kujitafutia kipato.

Rais alisema matumizi ya baruti katika uvuvi yamewafanya wavuvi kufuata samaki katika kina kirefu cha maji kwa kuwa wamekimbilia huko baada ya makazi yao kuharibiwa na baruti. Aliwataka viongozi wanaosimamia sekta hiyo mkoani Lindi kusimamia suala hilo ingawa anahisi nao wanahusika katika vitendo hivyo haramu.

**MAENDELEO DUNI**

Akiwa katika Kijiji cha Mitwero, Rais alisema kiwango cha maendeleo katika mkoa huo ni duni kulinganisha na fursa zinazopatikana yakiwano madini ya aina mbalimbali, bahari na misitu.

Aliwasisitiza wakazi wa mkoa huo kuongeza nguvu katika uzalishaji hasa katika uvuvi na kilimo cha mwani na serikali imeanza kusambaza vitendea kazi vya kisasa ili kuongeza kiwango cha mazao ya baharini.

Rais aliitaka Wizara ya Madini kuhamasisha vijana kushiriki katika uchimbaji wa madini kwa kuwa haoni sababu ya kundi hilo kutokuwa na ajira kwa rasilimali za kutosha zinapatikana mkoani humo.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema ujenzi bandari hiyo uliogharibu Sh. bilioni 280, unaonyesha nia na dhamira ya dhati ya Rais ya kuinua sekta ya uvuvi nchini.

Alisema ujenzi huo utaongeza fursa za kiuchumi wa Kilwa na kanda ya kusini kupitia uwekezaji na kuongeza mchango wa sekta kwa taifa kutoka asilimia 1.8 ya sasa hadi 10 ifikapo mwaka 2036.

Ulega pia alisema bandari hiyo itakuwa na karakana ya kutengeneza meli na nyavu za kuvulia samaki, hivyo kuondoa gharama za kuagiza nje ya nchi.

Pia alisema bandari hiyo uwezo wa kupokea meli 10 zenye ukubwa wa mita 30, eneo la kuhifadhi samaki tani 90 walioganda na walioyeyuka tani 1,300 kwa wakati mmoja hivyo kutoa ajira kwa vijana takribani 30,000.

Alisema boti 160 zinazotolewa kwa wavuvi na wanawake zitawawezesha kuvua samaki na kulima zao la mwani kwenye maji ya kina kirefu na kuondoa changamoto waliyokuwa nayo muda mrefu na kurudisha nyuma juhudi za kuletea maendeleo.

## Msomi mwenye shahada tisa afariki dunia

**Na Romana Mallya**

MSOMI nguli na Ofisa Msimamizi Mkuu wa Fedha Daraja la Kwanza katika Wizara ya Fedha, Prof. Handley Mpoki Mafwenga, ambaye alijizoelea umaarufu kwa kutangaza kuwa ana shahada tisa, amefariki dunia.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dk. Natu Mwamba, ilisema Prof. Mafwenga aliyekuwa akifanya kazi katika Ofisi ya Kamishna wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP), alifariki dunia usiku wa kuamkia jana katika Hospitali ya Taifa (MNH) alikokuwa akipatiwa matibabu.

Wakati akichukua fomu kugombea Uspika wa Bunge, aliushangaza umma baada ya kujitangaza kuwa ana shahada tisa, zikiwamo mbili za uzamivu (PhD) katika masuala ya fedha na sheria.

Licha ya kuwa na shahada hizo, msomi huyo aliweka bayana azma yake ya kuongeza shahada nyingine huku kadi yake ya utambulisho (business card) ikiwa imejaa shahada hizo ambazo amezisomea.

Akizungumzia wakati huo akichukua fomu ya kugombea uspika mwaka jana, Prof. Mafwenga alisema: "Nina degree zangu tisa. Nina Masters of Science of Finance (shahada ya umahiri katika masuala ya fedha) ya Scotland. Tulivaa sketi wakati tunahitimu."

Historia yake ya elimu inaonyesha kuwa baada ya kumaliza kidato cha nne, alisoma cheti cha uhasibu na akaajiriwa kwa sifa hiyo.

Baada ya kufanya kazi kwa muda, alijiunga na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) akisomea Stashahada ya Juu (Advanced Diploma) ya masuala ya kodi kisha stashahada ya uzamili (PGD) pia katika masuala ya kodi.

Alifanya shahada ya uzamili katika usimamizi wa fedha kutoka Chuo Kikuu cha Strathclyde, Scotland na baadaye Shahada ya Uzamivu (PhD) katika fedha. Katika sheria pia alisoma kuanzia degree ya kwanza hadi ya uzamivu (PhD) huku akiwa na shahada mbili za uvamili. Prof. Mafwenga aliwahi kusema wakati mwingine alilazimika kusoma shahada mbili kwa wakati mmoja.

Prof. Mwafyenga pia amewahi kugombea ubunge wa Afrika Mashariki mara mbili kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) bila mafanikio.

Mbali ya usomi aliokuwa nao, kwa nyakati tofauti ameshakuwa mshereheshaji (MC) na amewahi kuwa mwandishi wa habari kwa kuandika nakala katika magazeti mbalimbali.



HABARI KITAIFA

# Manispaa Temeke yajiandaa kuikabili mvua ya El-Nino

Na Elizabeth Zaya

KUTOKANA na taarifa ya ujio wa mvua ya El-Nino iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) Julai, mwaka huu, Wilaya ya Temeke imeanza kuchukua hatua kwa kuandaa na kusafisha mitaro ya kupitisha maji.

Mkuu wa wilaya hiyo, Mobhare Matinyi alisema jana wakati akizindua wiki ya usafi iliyofanyika Kurasini, wilayani humo.

Matinyi alisema, manispaa hiyo imeanza kufanya usafi wa mfereji wa Serengeti ambao ni miongoni mwa mikubwa wilayani humo.

Alisema maandalizi ya mfereji huo yamegharimu Sh. milioni 15 na wanaamini utakuwa msaada mkubwa katika kipindi hicho.

"Kipaumbele kingine ni kufanya usafi katika masoko yote, sehemu za biashara na kwenye maeneo ya makazi. Hii itakuwa ni wiki ya kipekee ambapo usafi utafanyika kwa wiki zima na lengo likiwa ni wilaya na manispaa kwa ujumla inakuwa safi, lakini pia kuufanya usafi kuwa tabia kwa wananchi wa eneo hili," alisema Matinyi.

Julai 19 mwaka huu, TMA, ilitoa taarifa ya kutahadharisha matarajio ya uwapo wa mvua ya El-Nino katika kipindi cha msimu wa vuli kuanzia Oktoba hadi Desemba, mwaka huu.

Miongoni mwa maeneo yaliyotajwa na TMA yatakayoathirika na El-nino ni mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara.

Matinyi aliwataka wananchi kuongeza juhudi katika usafi na kutunza mazingira ili kuokoa fedha nyingi ambazo hutumika kurekebisha miundombinu inayoharibiwa na uchafu.

"Suala la usafi si la siku moja tu, ni endelevu na uongozi umeweka vipaumbele ikiwamo kuhakikisha mifereji na mitaro inazibuliwa ili kuruhusu maji kupita kwa urahisi hususani wakati wa mvua za El nino zitakazoanza mapema mwezi ujao kulingana na taarifa za TMA," alisema Matinyi.

# Muhimbili yafanya upasuaji wa kifua kwa tundu dogo

Na Mwandishi Wetu

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imefanya upasuaji wa kwanza wa kifua kwa mgonjwa ili kuondoa uvimbe katika pafu kwa kutumia tundu dogo.

Upasuaji huo umefanywa na wataalamu wazalendo, wakiongozwa na Bingwa wa Upasuaji Kifua Duniani na mgunduzi wa upasuaji wa aina hiyo, Dk. Diego Gonzalez Rivas kutoka Hispania.

Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji (MNH), Dk. Rachel Mhaville, alibainisha jana kuwa upasuaji huo ni mwendelezo wa azma ya serikali chini ya Wizara ya Afya kuhakikisha huduma za kibingwa na ubingwa bobezi zinatolewa nchini.

"Zinaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza kutumia tundu moja dogo kupitia hospitali ya umma katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kulinganisha na matundu matatu yaliyozoeleka sehemu nyingine duniani," alisema.

Mkuu wa Idara ya Upasuaji MNH Upanga, Dk. Ibrahim Mkoma, alisema mgonjwa akifanyiwa upasuaji huo ambao siyo wa kufungua kifua, anaweza asihitaji kukaa Chumba za Uangalizi Maalum (ICU) kama wagonjwa wengine wa upasuaji wa kawaida na akaruhusiwa siku ya pili au ya tatu, hivyo kuendelea na shughuli zake mapema zaidi.

Dk. Mkoma alisema wagonjwa wapatao wanne wanategemewa kufanyiwa upasuaji wa aina hiyo na baada ya hapo, watalaamu wazalendo wataendelea kutoa huduma hiyo kwa wananchi wenye changamoto mbalimbali.

# TANESCO yatangaza rasmi ratiba upatikanaji umeme

Na Elizabeth Zaya

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limetoa ratiba ya upatikanaji umeme katika kila eneo, kutokana na upungufu wa nishati hiyo kutoka vyanzo vyake vya uzalishaji.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, Mkoa wa Dar es Salaam ni miongoni mwa itakayokumbwa na tatizo hilo la umeme ambalo litafanyika kwa kupishana kwa saa kadhaa.

Baadhi ya maeneo umeme utakatwa kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 12 jioni na sehemu nyingine ni kuanzia saa 12 jioni hadi saa sita usiku.

Nipashe imepata ratiba za baadhi ya maeneo hayo ambayo ni Kinondoni Kusini, Kaskazini na Temeke ambayo inaonesha kuanza tangu juzi hadi Jumamosi ijayo.

Taarifa hiyo inaonesha ratiba hiyo itakuwa inapishana kwa kila eneo kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 12 jioni, siku inayofuata litakata nishati hiyo kuanzia saa 12 jioni hadi saa sita usiku. Ratiba hiyo pia imehusisha Mkoa wa Iringa.

Ufafanuzi wa TANESCO ulioutoa mwishoni mwa wiki kwa gazeti hili ni kwamba hali hiyo ya ukatikaji umeme siyo mgawo, bali inatokana na upungufu wa huduma hiyo katika vyanzo vya uzalishaji.

Baadhi ya wadau waliozungumza na gazeti hili walisema hali hiyo ya kukosekana kwa umeme imewarudisha nyuma katika shughuli za uzalishaji.

"Kwa mfano mimi shughuli yangu ninategemea umeme kufua vyuma, kwa hiyo ninapokuwa na zamu ya kukosa huduma kuanzia asubuhi mpaka jioni naathirika sana kwa sababu nategemea shughuli hii kuendesha familia," alisema Jastine Nkami mkazi wa Bunju A.

"Ifike mahali Tanesco ikiri kwamba huu ni mgawo na siyo upungufu, wasituchanganye sisi wateja wao kwa kutumia lugha laini wakati hata hivyo sisi ndiyo tunaoathirika, kwa mtindo huu hali itazidi kuwa mbaya kama hakuna hatua za haraka zitakazochukuliwa kunusuru," alisema.

Nkami alisema wana marejesho ya mikopo ambayo bila kuingiza kipato chochote kwa siku ni vigumu kuirejesha na kuhudumia familia.




# Dk. Anna Henga: Hiki ndicho kinanifurahisha kwa Samia

## Asimulia anavyoishi; mama nyumbani, mchungaji kanisani, bosi na mwanasheria... dereva wake mwanamke



Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga..

**JINA Dk. Anna Henga, bosi mkuu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, ni kubwa kupitia wajibu wake - kutetea haki za umma na mustakabali wa kinamama. Je, mwanasheria huyo anaishi vipi, kazi zake na maisha yake ya kila siku yanayoashiria matendo yake?**

**Simulizi yenye undani wake, iko katika mazungumzo ya ana kwa ana na waandishi wa makala hii. Fuatilia sehemu ya kwanza:**

**Swali:** Kipi kinakufurahisha katika uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan na kipi hakikufurahishi?

**Dk. Anna:** Nimependa Rais Samia ambavyo amekuja na zile R4 ambazo kwa Kiswahili ni maridhiano, ustahimilivu, kujenga upya na upatanishi kwa nia ya kutaka tusahau ya zamani na machungu ya miaka sita iliyopita na kujenga nchi yetu.

Leo Rais tunamwita kwenye matukio yetu anakuja. Tunamwomba kumwona anatukaribisha. Kwa hiyo, ni suala la kutaka kwenda kuomwona Rais kwa ajenda hii na anakubali. Zamani haikuwa hivyo.

Kitu ambacho hakinifurahishi ni hawa watu ambao wanaitwa chawa ama wanajiita watetezi wa mama. Wavuruga!

Mimi ninaweza kusema wanamvurugia kwa sababu nia yake na matendo yao ni tofauti, kwa sababu yeye ana nia ya kujenga ila wao wanabomoa zaidi. Kwahiyo, angeweza kukemea hao chawa ingejenga zaidi.

**Swali:** Jeshi la Polisi lilichukua vifaa vyenu vya kazi kwa tuhuma za kujihusisha na kuhesabu kura za Uchaguzi Mkuu. Je, vifaa vilirudishwa? Iliathiri vipi utendaji wenu wa kazi?

**Dk. Anna:** Vifaa vyetu vilirudhishwa na kesi tuliyofunguliwa inatokea kifungu cha 16 ya Sheria ya Makosa ya Mtandaoni. Sheria hiyo imechanganua makosa mbalimbali kwa upana.

Hawakutufungulia kesi kwa makosa ya tulihesabu kura. Kuhesabu kwenye sheria si kosa la jinai, japokuwa sisi hatukufanya hivyo, lakini tulikuwa tunafuatilia tu uchaguzi, na si kosa kisheria.

Ninadhani ilikuwa ni vigumu kutufungulia makosa hayo na baadaye waliona hatuna hatia na wakaturudishia vifaa vyetu. Vifaa vilirudishwa japo vilikaa miezi minane na vingine vilikuwa vimeharibika, lakini vyote tulipatiwa. Kwa vifaa vilivyoharibika hakuna fidia yoyote tuliyopata na tulipaswa kufungua kesi, lakini ninadhani ilikuwa ni muda mrefu karibia miaka saba sasa. Sina rekodi kama tulifungua ama hatukufungua, ninachokumbuka ni kwamba nilikuwa ninasimamia kile kituo na vifaa vyetu vyote vilirudi.

Lakini ni ukweli kwamba ilituathiri maana tulichelewa kuwasilisha ripoti. Na ripoti yetu inapaswa kuwasilishwa 'online' (mtandaoni), na kama unavyojua siku hizi ripoti haziandikwi kwenye karatasi.

Lakini pia tulipelekwa mahabusu na tutakaa hadi usiku wa manani na familia zetu pia ziliathirika.

Ukiwa mwanaharakati wa haki za binadamu, hayo mambo hutokea kwa sababu unaonekana kama unapinga au unafanya kinyume, lakini baadaye wakiona unafanya kitu sahihi wanakuachia.

**Swali:** Unawezaje kujigawa - mkurugenzi wa taasisi, mama nyumbani na kiongozi kanisani na vyote vikaenda bila kuathiriana?

> **Dk. Anna: Ni kweli dereva wangu ni mwanamke na kuhusu ilitokeaje, ni mimi nilipendekeza ofisi yangu kuwa na wanawake wengi zaidi kulinganisha na awali...**

**Dk. Anna:** Inabidi kuongeza muda wa kufanya majukumu yangu, lakini kugawana kazi kwa sababu huwezi kufanya kila kitu bila msaada. Kwahiyo, wasaidizi wangu wananisaidia katika hilo wakiwamo wa hapa ofisini, nyumbani na walimu shuleni ili kuhakikisha kila kitu kinakwenda sawa.

**Swali:** Wewe ni miongoni mwa viongozi wachache wa taasisi kubwa ambao madereva wao ni wanamke. Kuna nini nyuma ya uamuzi huu?

**Dk. Anna:** Ni kweli dereva wangu ni mwanamke na kuhusu ilitokeaje, ni mimi nilipendekeza ofisi yangu kuwa na wanawake wengi zaidi kulinganisha na awali, lakini sipendezwi na hali ya watu au jamii kudharau jinsi moja na kupenda nyingine.

Kwenye kitengo cha dereva, haikuwa rahisi ofisi yangu kunielewa. Wapo waliokuwa wanasema 'utapata ajali, mwanamke ataharibu gari', lakini mwisho dereva niliyemchagua alikuwa na vigezo vyote kama walivyonavyo wanaume.

Ni dereva mwenye leseni ya udereva kutoka Chuo cha Usafirishaji. Kwahiyo, nikampitisha yeye kuwa katika nafasi hiyo na sasa ni mwaka wa tatu toka nianze kufanya naye kazi.

**Swali:** Katika kipindi chako cha uongozi, ni misukosuko gani umeshawahi kupitia ambayo ni ya kipekee zaidi?

**Dk. Anna:** Kila kazi ina misukosuko na changamoto zake. Hata kama ni kazi ya dini - unawahubiria watu kwenda mbinguni, lakini lazima upate changamoto.

> **Taasisi na vyombo vya dola vifanye kazi yake, serikali ifanye kazi yake. Mahakama ifanye kazi yake ya kutetea kwa haki na Bunge lifanye kazi yake ya kuisimamia serikali ili kuleta haki kwa wananchi ikiwamo haki ya maendeleo na haki nyinginezo.**

Misukosuko mingi inatokea hasa pale watu wanapokosa uelewa wa masuala ya asasi za kiraia hasa asasi za utetezi wa haki za binadamu.

Wanadhani tunataka kuipinga serikali wakati wote, kumbe serikali ingetupenda zaidi kwa sababu tunawasaidia zaidi kuleta amani na kusaidia watu kufikia haki.

Lakini bado tunaendelea kufanya kazi na serikali na kushirikiana na wananchi na vyombo vyote vilivyopo nchini.

**Swali:** Ni sekta ipi ina mafanikio zaidi na ipi ina matatizo zaidi katika maeneo ambayo LHRC inayamulika?

**Dk. Anna:** Kwa sekta zilizofanikiwa nitatolea mfano kwenye elimu. Idadi ya watoto wanaojiunga katika shule za msingi ni kubwa hasa kwa wasichana, lakini sekta ya elimu inatakiwa ifanye utafiti zaidi kwanini kila ngazi ya elimu inavyozidi kupanda wanazidi kupungua, na sisi kazi yetu sio kutatua bali kuandika ripoti na kupeleka katika sekta husika ili waifanyie kazi.

**Swali:** Taasisi yako imekuwa ikifanya utafiti kuibua haki za binadamu na sheria za kitaifa na kimataifa. Je, unaridhishwa na utekelezaji wa mapendekezo ya taasisi yako kwa serikali?

**Dk. Anna:** Ninaridhika nayo sana kwa sababu mengi yanafanyiwa kazi na ambayo hayafanyiwi kazi tunapeleka mwaka unaofuata. Kwa ujumla yanakuwa ni ya haki za binadamu, haki za makundi ya kijinsia na mengineyo.

Kwa kawaida haki huwa inahitajika kwa siku zote, ndio maana maono yetu ni kwenye jamii, haki na ustawi, pia tunatamani siku zote haki zinatakiwa ziheshimike.

Taasisi na vyombo vya dola vifanye kazi yake, serikali ifanye kazi yake. Mahakama ifanye kazi yake ya kutetea kwa haki na Bunge lifanye kazi yake ya kuisimamia serikali ili kuleta haki kwa wananchi ikiwamo haki ya maendeleo na haki nyinginezo.

Kwahiyo, mara nyingi hali inavyokuwa na inakuwa sivyo tunavyotaka, kama kuna haki zinazovunjwa na kwa wakati huohuo tunatetea, tunafuatilia lakini tunasema hapana pale ukiukwaji unapofanyika.

Na inaposhindikana kwa wakati huo tunapeleka mwaka ujao kwa ajili ya ripoti na tunasema 'haya hayajafanyika' na nini kifanyike ili kuleta haki kwa wananchi.

**Swali:** Wakati unaingia madarakani uliachiwa majukumu na malengo ya mtangulizi wako, Dk. Hellen. Tueleze utekelezaji wake na kama kuna uliyoongeza.

**Dk. Anna:** Ni miaka mingi sana, takribani miaka mitano na huu ni mwaka wa sita sasa na ingalikuwa ni kipindi cha urais au ubunge ni awamu moja sasa imepita.

Lakini ni mambo mengi yameendelea na mafanikio ni mengi kuliko changamoto na pia tumekuwa na mabadiliko katika uongozi na hata katika ngazi ya nchi. Kwa hiyo, hata siasa na mambo ya haki pia yamebadilika, lakini tunaendelea vizuri.

Pia shirika limeendelea vizuri zaidi kutokana na mtangulizi wangu naye aliliendesha vizuri kwa miaka aliyokuwa amekaa.

**Swali:** Uendeshwaji wa taasisi ni gharama. Vyanzo vyenu vya mapato kujiendesha vinatokana na nini?

**Dk. Anna:** Vyanzo vya mapato yetu ni michango ya wanachama na michango ya wahisani mbalimbali zikiwamo taasisi za Umoja wa Mataifa.

Hivyo, mtu yeyote mwenye mapenzi mema, anaweza akachangia kazi zetu na kwenye tovuti yetu tumetoa namba za kuchangia, pia unaweza kuchangia zaidi kwa kuwa mwanachama wa kituo, itatusaidia sana kuendeleza malengo yetu.

***Imeandaliwa na Mwanahamisi Mussa na Emmaloveness Gaston (TUDARCo)**

**FUATILIA SEHEMU YA PILI KESHO**

## HABARI KITAIFA

# Taasisi yabaini dosari miundombinu ya elimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya WAJIBU kupitia mradi wa uwajibikaji (AAI) imebaini masuala kadhaa katika miundombinu ya sekta ya elimu nchini, ikitoa mapendekezo sita.

Mapendekezo hayo yanajumuisha serikali itilie mkazo utekelezaji wa hoja za Ripoti za Wathibiti Ubora baada ya kubaini zinafungiwa kabatini.

Jana katika mkutano wa uwasilishaji wa Taarifa ya Hali ya Elimu, Meneja miradi kutoka taasisi hiyo, Moses Kimaro, alisema jijini hapa kuwa wamebaini mapendekezo ya wathibiti ubora yamekuwa hayafanyiwi kazi kama ilivyo kwa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema katika shule nne za msingi za Mindola na Chilungulu wilayani Bahi na Lipupu na Magomeni za Nanyumbu, matokeo ya ripoti za kamati za ufuatiliaji jamii (PETs) yameonesha kwa miaka miwili mapendekezo ya Mthibiti Ubora wa Shule hayakutekelezwa.

"Kwa mfano, asilimia 82 ya mapendekezo kuhusu upungufu wa madarasa hayakutekelezwa, asilimia 100 ya mapendekezo kuhusu upungufu wa nyumba za walimu hayakutekelezwa, asilimia 100 ya mapendekezo kuhusu upungufu wa vyoo hayakutekelezwa," alisema.

Kimaro alipendekeza Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, waziagize halmashauri kuwa na mpango mkakati wa utekelezaji mapendekezo ya Mthibiti Ubora wa shule ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa mapendekezo hayo.

"Vilevile, ihamasishe kamati za shule kupitia mipango hiyo ili kudai uwajibikaji wa utekelezaji wake kwa wakati, kuwe na vikao vya mara kwa mara vinavyohusisha Mthibiti Ubora na halmashauri ili kupitia mapendekezo hayo na Ripoti ya Mthibiti Ubora na CAG kuwa ajenda ya kudumu katika vikao vya halmashauri na vijiji.

"Kuna ripoti wathibiti wamezitoa kwenye shule na halmashauri, lakini zimefungiwa na wala hakuna mtu wa kuuliza utekelezaji wake. Kwahiyo, zinafungiwa tu, lakini zina mambo mazuri kuhusu miundombinu na zinatoa mapendekezo.

"Hawa wathibiti hawashirikishwi hata kwenye ujenzi wa miundombinu na badala yake wanatumika tu kwenye kuthibitisha usajili, wanathibitisha kwenye majengo ambayo tayari yameshajengwa," alisema.

Kuhusu upangaji na upatikanaji fedha, Kimaro alisema TAMISEMI inapaswa kutoa kipaumbele katika upangaji na upatikanaji rasilimali fedha kwa shule zenye hali mbaya ya miundombinu kwa kuzingatia ripoti ya CAG, ripoti ya Mthibiti Ubora wa Shule wa Wilaya na ripoti ya tathmini ya mahitaji ya shule.

"Kwa mfano, katika Halmashauri ya Nanyumbu, Shule ya Mangaka imekuwa inapokea fedha kwa kipindi cha miaka mitatu zenye maelekezo kuwa zitumike katika ujenzi wa vyoo tu. Sh. milioni 32 (2019/20), Sh. milioni 66 (2022/23) na Sh. milioni nane (2023/24)," alifafanua.

Alibainisha kuwa Ripoti ya Mthibiti Ubora wa Shule ilionesha upungufu wa vyumba 18 vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi 1,425 kwa uwiano wa 1:45 na baadhi ya vyoo vilivyojengwa havitumiki kutokana na ukosefu wa maji.

Kuhusu ujenzi wa maboma unaotekelezwa kwa jitihada za jamii, Kimaro alisema taasisi yao inashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI ikamilishe jitihada za jamii kwa mujibu wa mwongozo uliopo. "Mfano, katika Mkoa wa Mtwara, Halmashauri ya Nanyumbu wananchi wamejenga maboma 70 hadi kwenye lenta na yamebaki bila kukamilishwa kwa zaidi ya miaka minne.

"Jambo hili pia linaoneka katika Wilaya ya Tanganyika Mkoa wa Katavi ambako wananchi wamejenga maboma 214 hadi kwenye lenta na yamebaki hivyo kwa zaidi ya miaka mitatu," alisema.

Alishauri serikali kuanzisha mkakati wa ukamilishaji wa maboma katika ngazi ya halmashauri na fedha ikipatikana kipaumbele cha wananchi kizingatiwe.

Kadhalika, Kimaro alisema WAJIBU inapendekeza TAMISEMI izingatie muda stahiki wa ujenzi ili kuepuka ujenzi wa miundombinu chini ya kiwango.

"Katika Halmashauri ya Mji wa Makambako, Shule ya Msingi ya Azimio ilitengewa Sh. milioni 347.5 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba tisa vya madarasa, matundu 16 ya vyoo, jengo la utawala na sehemu ya kuchomea taka hatarishi. Shule ilipokea fedha hizo tarehe 26/04/2023 na kutakiwa kukamilisha ujenzi tarehe 4/07/2023,"alisema.

Vilevile, alisema katika Halmashauri ya Tanganyika, Shule ya Kasekese ujenzi ulitakiwa kuanza tarehe 01/4/2021 na kukamilika tarehe 15/06/2023, huku kiuhalisia walianza ujenzi tarehe 20/5/2023 na kukamilisha tarehe 09/8/2023.

"Katika Halmashauri ya Tanganyika, Mwalimu Mkuu wa Shule alipokea maelekezo kutoka mamlaka ya halmashauri kutoa fedha kwenye akaunti ya shule na kuziweka kwenye akaunti ya TAPSHA kwa ajili ya kugharamia maandalizi ya mitihani na michezo," alisema.

Alibainisha kuwa fedha za 'capitation' zinazopelekwa shuleni zinatumika kulingana na fomula ya matumizi ya ruzuku na bajeti iongezwe kulingana na rasilimali watu.

Awali, Ofisa kutoka taasisi hiyo, Tekla Mleleu, alisema mradi huo wa uwajibikaji umefanyika kwa kushirikiana na taasisi za MTWANGONET, NGONEDO, UDESO na SHIPO katika Halmashauri za Nanyumbu, Bahi, Tanganyika na Makambako.

## Raia wa Marekani kortini tuhuma za kujipatia kitambulisho cha NIDA

**Na Grace Gurisha**

RAIA wa Marekani, Yaki Juma, amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam akikabiliwa na mashtaka matano likiwamo la kutoa taarifa za uongo na kujipatia Kitambulisho cha Taifa (NIDA).

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali kutoka Idara ya Uhamiaji, Godfrey Ngwijo, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Evodia Kyaruzi kuwa raia huyo alitenda kosa hilo Septemba, 2023.

Ngwijo alidai kuwa katika shtaka la kwanza mshtakiwa anatuhumiwa Septemba 14, mwaka huu akiwa katika Ofisi za Uhamiaji, Ilala, Dar es Salaam, alikutwa akiishi nchini bila kibali.

Katika shtaka la pili, alidai kuwa katika tarehe na eneo hilo, mshtakiwa raia wa Marekani, alitoa taarifa za uongo kwa maofisa Uhamiaji, kuhusu utaifa wake kwa lengo la kujipatia hati ya kusafiria ya Tanzania.

Ilidaiwa kuwa katika shtaka la tatu, mshtakiwa tarehe hiyo na eneo hilo, aliwasilisha nyaraka za kughushi kwa lengo la kujipatia cheti cha kuzaliwa na kadi ya Taifa la Tanzania.

Katika shtaka la nne alidai kuwa mshtakiwa huyo alitoa taarifa za uongo kuhusu uraia wake kwa lengo la kujipatia kadi hiyo.

Aidha, inadaiwa kuwa mshtakiwa huyo alifanikiwa kupata kadi ya Taifa la Tanzania kwa njia ya udanganyifu.

Mshtakiwa alikiri shtaka la kuishi nchini bila kibali na kukana mashtaka mengine.

Ngwijo alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuiomba Mahakama ipange tarehe nyingine kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa hoja za awali.

Mshtakiwa alirudishwa mahabusu baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana ya kuwasilisha mahakamani hapo hati yake ya kusafiria pamoja na wadhamini wawili wenye vitambulisho vinavyotambulika kisheria.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Septemba 22, mwaka huu kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa hoja za awali.



Mkazi wa Kijiji cha Mikwamba, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Eveline Zuberi (68), akiponda kokoto ili kupata ujira wa siku kijijini hapo jana. Aliomba kwa wasamaria wema kumsaidia kuongeza mtaji wa kukuza biashara yake hiyo. Kulia ni mkazi wa eneo hilo, Fred Shedafa. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mwili wa mwanamume aliyemkata koromeo mpenzi, haujatambuliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma limesema hadi sasa mwili wa mwanamume aliyefahamika kwa jina moja la Amosi, anayedaiwa kumuua mpenzi wake kwa kumkata koromeo na kisu, hakuna ndugu aliyejitokeza kuutambua.

Mwanamume huyo anayejishughulisha na shughuli za ujenzi jijini hapa, anadaiwa kumuua mpenzi wake Samira Mathiasi kwa kumkata koromeo kisha kujichoma kisu tumboni kwa kinachodaiwa kuwa ni wivu wa mapenzi.

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa nane usiku katika eneo la Oysterbay, Kata ya Makulu, ndani ya chumba alichokuwa amepanga mwanamke huyo.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Dodoma, Martin Otieno, alisema mwili wa mwamume huyo umehifadhiwa katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma.Kamanda Otieno alitoa wito kwa wananchi kujitokeza kuutambua mwili huo ili hatua nyingine ziendele.

"Watu waje wautambue mwili huu ili hatua nyingine zichukuliwe, lakini nitowe wito kwa wananchi kuwa watu wanaofanya nao kazi wanawafahamu kwa majina, lakini pia kutambua shughuli wanazozifanya ili kuepusha usumbufu kama huu ambao unatokea hivi sasa," alisema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Msangalale Magharibi lilipotokea tukio hilo, Leonard Shamba, alisema mwili wa mwanamke huyo ulichukuliwa juzi usiku na ndugu zake.

Mama mzazi wa marehemu Samira, Rachel Izengo, juzi wakati wa maandalizi ya kusafirisha mwili wa mwanawe alisema jina la mtoto wake ni Esther Ramadhan Isugilo na siyo Samira Mathias lililozoeleka mtaani hapo.

Alisema taarifa za kifo cha mtoto wake amezipata kupitia kwa majirani zake saa 10 usiku wa kuamkia juzi akiwa mkoani Shinyanga ambako ndiko anaishi.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo aliaanza safari muda huo na kufika jijini Dodoma majira ya saa nane mchana juzi ili kujua sababu ya kifo cha mwanawe ambaye ndiye wa kwanza kati ya watoto watatu alionao.

"Nimesikitishwa sana na kifo cha mwanangu cha kuchinjwa, sikutarajia kama atakufa kifo kama hichi binti yangu alikuwa ni mtu wa watu," alisema huku akilia kwa uchungu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Huduma Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inufaishe wengi

**WANANCHI** 280,954 kutoka mikoa ya Ruvuma, Shinyanga, Dodoma, Manyara na Simiyu wamefaidika na huduma ya msaada wa kisheria iliyoanza kutekelezwa rasmi mwezi Aprili, mwaka huu.

Jumla ya idadi hiyo ya wananchi imefaidika na huduma hiyo baada ya kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ilipoanza.

Idadi hiyo ilitangazwa na Waziri wa Katiba na Sheria Dk. Pindi Chana alipokuwa akizindua rasmi kampeni hiyo katika mji wa Bariadi, ambaye anasema idadi kubwa ya wananchi wanaojitokeza kupata huduma hiyo ni wanawake.

Imeelezwa kuwa hadi sasa wananchi 280,954 wamefikiwa na kampeni hiyo wakiwamo wanawake 149,934 na wanaume 139,020 kwenye mikoa ambayo kampeni hiyo imezinduliwa.

Hii inaonesha kuwa wananchi wengi wanahitaji msaada wa kisheria, lakini wanakosa wapi kwa kuanzia.

Mwitikio huo wa wananchi unaashiria kuwa kuna matukio mengi katika jamii ambayo yanafanyika na kukiuka sheria na wananchi wengi wakibaki wanadhulumiwa haki zao.

Kwa takwimu zilizotolewa, inaonesha wanawake ndiyo wanahitaji sana msaada wa kisheria kutokana na wengi kudhulumiwa haki zao hasa inapotokea ameondokewa na mwenza wake.

Kinamama wengi hunyang'anywa mali na ndugu wa mume na mama kuachwa akihangaika na watoto wake na anapotaka kufuatilia haki zake anakumbuna na milolongo ambayo humkatisha tamaa na kumwachia Mungu afanye uamuzi wake.

Waziri Chana anabainisha kuwa kampeni hiyo imesaidia kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaotafuta huduma za msaada wa kisheria katika maeneo yao kupitia uwakilishi mahakamani, ushauri wa kisheria na utatuzi wa migogoro.

Kadhalika, kampeni hiyo imesaidia kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa kuwa wananchi wamepata uelewa wa masuala ya haki za binadamu na ulinzi wa makundi maalum na kuibuliwa kwa migogoro ya muda mrefu.

Kuanzishwa kwa kampeni hiyo kumesaidia kutatuliwa kwa malalamiko kwa njia mbadala na hivyo kuimarisha amani kati ya pande zote zilizokuwa na migogoro.

Katika maeneo ya vizuizi, kampeni hiyo imesaidia wafungwa na mahabusu kupata uelewa kuhusu haki zao na wapo waliopata dhamana na rufani zao kusikilizwa na hatimaye wapo waliachiwa baada tu ya kupata huduma za msaada wa kisheria.

Kampeni hii imeonesha jinsi wananchi wanavyohitaji elimu ya kujua haki zao na pia namna ya kupambana kuondoka na uonevu.

Wananchi waliopo katika Mkoa wa Simiyu na mikoa jirani ambako kampeni hiyo imezinduliwa ni muhimu wakajitokeza kwa wingi ili wanufaike na msaada wa kisheria ambao unatolewa bila gharama yoyote kwa kuwa Rais Samia ameshatoa fedha za kuwawezesha wataalamu kutoa huduma hiyo bila malipo kwa wananchi.

Ni muhimu pia kampeni hii ikazinduliwa nchi nzima ili wananchi wengi wapate uelewa wa haki zao kisheria na wanapoona kuwa sehemu fulani hawajatendewa haki waweze kujipigania kwa kufuata utaratibu uliowekwa.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nwanda, wananchi wa mkoa huo wamehamasika mjini na vijijini kupata huduma ya msaada wa kisheria.

Kuhamasika kwao kumewafanya wajitokeze kwenye uzinduzi wa kampeni kwa lengo la kupata huduma hiyo ambayo imekuwa ni tatizo kubwa kwa wananchi.

Ni matumaini yetu kuwa kampeni hiyo itawasaidia wananchi kupata uelewa wa sheria ili kupunguza migogoro katika jamii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Tuntule Swebe

# Ushirikina huu jamani hausaidii

**IMEKUWA** ni kawaida watu hasa vijana kutamani maisha bora, kama nyumba za kifahari, magari ya gharama kubwa na starehe za hali ya juu hata bila kujali vinapatikanaje.

Ndiyo maana kuna matukio au tabia za kutangaza kupata utajiri kupitia mbinu hatarishi vijijini na hata mijini, wateja wakitangaziwa kuwa watatajirika kwa kuhudumiwa na waganga wenye uwezo wa kuwapa mali na utajiri kwa haraka, kung'arisha nyota, kuongeza mvuto kwa wenza na kuunganishwa na mamilionea au Free Masons.

Wapo wengine wanaoingia kwenye makundi ya uhalifu wakiamini watafanikiwa kimaisha na hawatabainika kwa kutumia hirizi, mazindiko na hata mbinu nyingine za kuchanjiwa au kunyweshwa dawa.

Lakini ukweli ni kwamba matokeo yake yanakuwa kinyume na walivyotarajia kwa vile hakuna mafanikio.

Ukweli ni kwamba kutamani utajiri lakini kutumia mbinu za waganga na wataalamu wa hirizi lakini huna mipango wala hufanyikazi ni sawa na mbio za sakafuni huishia ukingoni na za mwizi ni arobaini.

Kutamani utajiri bila kufanyakazi kulisababisha pia mauaji ya watu wasio na hatia wanaoishi na ualbino vikichukuliwa viungo vyao ni chanzo cha utajiri yote haya yakiharibu sifa za Tanzania ndani na nje ya mipaka.

Wanaoishi na 'albinisim' walitishiwa na maisha yao yalikuwa hatarini na wakitafutwa ili kuuliwa na hao wasaka utajiri.

Tatizo la kutamani utajiri kupitia ushirikina linadaiwa kugusa hata wasomi nao huenda kwa waganga ili kupata shahada, kupanda vyeo, kutajirika haraka na wanapofika huko wanatamani kufanikiwa.

Wanachotumia ni mbinu mbalimbali kama kuua wenza, watoto wao na jamaa, wazazi na majirani kisa kupata pesa, lakini hakuna aliyetangazwa kuwa bilionea.

Mauaji yalisikika zama za kuua wazee kwa madai kuwa ni wachawi mkoani Tabora, Mwanza, Shinyanga na ukanda wote wa Kanda ya Ziwa kwa imani kuwa wazee hao ni chanzo cha kurudisha nyuma maendeleo yao, maelezo wanayoyapata kwa waganga na wabashiri au wapiga ramli.

Tanzania ya ushirikina imekuwa changamoto hata watoto wadogo ambao usalama wao uko shakani kwani wengine wameripotiwa kubakwa, kuingiliwa kinyume cha maumbile, kulawitiwa, kuuawa na kuchukuliwa viungo vya siri.

Wakati umefika watu kubadilika na kuachana na kuua au kuwapa wenzao ulemavu kwa kisingizio cha kutafuta fedha au utajiri na maisha bora.

Wapo wanaopata ulemavu maisha kwa kile kinachosadikika ni kukatwa viungo ili kupata utajiri au kuwasingizia kuwa ni wanga au wachawi.

Ni wakati wa kufahamu kuwa zama hizi ni za sayansi na teknolojia na jamii ziamke na kuachana na imani zisizo na manufaa kama kupata fedha au kufaulu masomo kwa msaada wa waganga au viungo vya watoto wadogo.

Ukiingia kwenye mabasi ya mikoani kuna muziki, sinema na vichekesho kama inawezekana madereva waweke CD na flash za kupinga ushirikina, dawa za kulevya, kuua watu na mambo yote ya kihalifu wanayotishia usalama wa raia ili abiria wao wasikilize na kubadilika.

Aidha, kuna haja ya kuweka mabango ya kupinga na kukanusha madai ya kupata msaada kwa waganga yanayowekwa mitaani, kwenye nguzo za umeme, miti na hata kwenye madaraja.

Watanzania wahamasike na kuanza kuweka mabango pembeni ya matangazo hayo kukanusha ujumbe unaotolewa . Mfano, kutangaza simu na maelezo yanayoambatana kuwa yupo mganga kutoka Sumbawanga anayeweza kukupa utajiri, mvuto na ufaulu darasani.

Liwepo bango la kukanusha kuwa utajiri haupatikani kwa waganga ni kazi na tena kwa bidii na maarifa, kuvumilia, kujituma na kuheshimu haki za binadamu wengine.

Si kwa kuua watoto, wenza, wazazi au waume badala yake ni juhudi, kuthubutu, kujifunza mbinu za kisasa, kujitafakari na kujua wapi wanapokosea na kutumia sayansi na teknolojia kwa manufaa yako si vinginevyo.

Lakini waganga wanaohadaa watu kuwa wana ujuzi kumbe si kweli waache maana ni chanzo cha kuleta fujo kwenye jamii, kukosekana amani, kuendeleza ujinga wafahamu kuwa wanakwenda kinyume na sheria na hata utaratibu wa maumbile.

Wahimizeni watu kulima, kufugaji, uvuvi, biashara ndogondogo, kuendesha boda, bajaji, ususi, upishi badala ya kuwarubuni na imani potofu kwamba

## TASAF kujenga stendi ya kisasa Peramiho

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, amezitaka Idara zinazohusika na ujenzi katika halmashauri kujenga stendi ya mabasi yenye ubora unaoendana na thamani ya fedha zilizotolewa ili kujenga stendi hiyo katika Kijiji cha Lundusi, Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma.

Alitoa agizo hilo wakati akizindua mradi wa ujenzi wa stendi ya kisasa ya magari katika kijiji hicho unaotekelezwa na Ofisi ya Rais kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), utakaogharimu Sh. milioni 482 ukitarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi sita tangu kuanza kwa mradi.

Alisema katika awamu ya kipindi cha pili cha utekelezaji, TASAF imejikita katika masuala ya kuwezesha kaya kutumia fursa za kukuza uchumi na kuongeza kipato kwa walengwa pamoja na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, elimu na majisafi na salama pamoja na miundombinu ya kukuza uchumi ngazi ya jamii.

"Wananchi wanasubiri stendi bora ya kisasa na siyo stendi mbovu, idara zinazohusika na ujenzi kwenye halmashauri sasa kumekucha na hatutarajii eneo la manunuzi ya ujenzi yakawa ni kichaka cha upotevu wa fedha kutoka Ofisi ya Rais kupitia Mfuko wa TASAF, hivyo matumizi sahihi ya fedha yadhihirishwe katika mradi huu," alisema.

Akitoa taarifa ya shughuli za TASAF katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Neema Maghembe, alisema kukamilika kwa ujenzi wa stendi hiyo ya mabasi utarahisisha usafiri kwa wananchi watakaofika kupata huduma.

"Faida nyingine ni mazingira bora kwa wafanyabiashara eneo la stendi, kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo la stendi kwa wasafiri na wafanyabiashara, kuongezeka kwa pato la halmashauri, kuongeza fursa ya ajira kwa vijana na wananchi pamoja na huduma ya usafiri kwa wanaosafiri kutoka nje na ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Shedrack Mziray, alisema mfuko huo umekuwa ukitekeleza miradi ya maendeleo nchini kwa lengo la kukwamua kaya maskini na hatimaye waweze kubuni na kuanzisha miradi yao binafsi ili kumudu gharama za maisha.

"Tunafanya utekelezaji katika maeneo manne kitaifa tunafanya uhawilishaji wa fedha ambapo mpaka sasa tumewasilisha Sh. bilioni 919.6 tangu kuanza kwa awamu ya kipindi cha pili mwaka 2020 na kufikia kaya zaidi ya milioni 1.3. Pia tumefanya miradi ya ajira za muda karibu miradi 14,236 yenye thamani ya bilioni 169 na kutoa ajira kwa kaya zaidi ya 660,000 pamoja na miradi ya kukuza uchumi wa kaya," alisema Mziray.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Vijijini, Menas Komba, aliishukuru serikali kwa kuendelea kutoa fedha kuhakikisha miradi mikubwa ya maendeleo inatekelezwa huku akiipongeza TASAF kwa kuanzisha mradi wa ujenzi wa stendi ya mabasi katika Kijiji cha Lundusi na kukamilika kwake kutainua vipato vya wananchi na taifa kwa ujumla.



Mkuu wa Wilaya ya Nzega, mkoani Tabora, Naitapwaki Tukai (wa pili kulia), akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Zacharia Mwansasu kwenye eneo la Ndala jana, ambapo utakimbizwa kwenye Halmashauri ya Wilaya hiyo na Mji wa Nzega. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mganga wa jadi aliyefungwa kifungo miaka 30 kwa kubaka ashinda rufani

**Na Kulwa Mzee**

MGANGA wa Jadi, Juma Issa, aliyefungwa miaka 30 jela kwa kosa la kubaka akidai anamwekea dawa binti sehemu ya siri, ameshinda rufani ya kupinga adhabu hiyo. Mahakama imeamuru aachiwe huru mara moja.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam mbele ya Jaji Elinaza Luvanda baada ya kukubali kwamba upande wa Jamhuri haikuthibitisha kosa bila kuacha shaka.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji Luvanda alisema mrufani ni mganga wa jadi na mwathirika ambaye ni binti (23), ni mteja wake aliyetambulishwa kwake na wazazi wake.

Mrufani inadaiwa alimfanyia twahara (kujisafisha na kujitakasa kutokana na uchafu) binti. Siku moja alimwambia kuna dawa anahitaji kumwekea sehemu ya siri. Binti alikubali kupata tiba. Mrufani akamwingilia.

Shauri hilo lilisikilizwa katika Mahakama ya Wilaya ya Temeke. Mahakama iliamini ushahidi wa shahidi wa kwanza na ikamtia hatiani mganga wa jadi huyo na kumhumu kifungo cha miaka 30 jela kwa kubaka.

Baada ya hukumu hiyo, mrufani aliwasilisha hoja nne Mahakama Kuu, akipinga hatia na adhabu aliyopewa na Mahakama ya Temeke.

Hoja zake ni: Utetezi wake haukuzingatiwa, taarifa ya daktari aliyefanya uchunguzi haikuonesha kulikuwa na ubakaji, ushahidi wa shahidi wa kwanza na wa pili unajikanganya na upande wa Jamhuri haikuthibitisha shtaka bila kuacha shaka yoyote.

Akijibu rufani hiyo, Wakili wa Serikali Agness Mtunguja, alidai mazingira ya kosa yalihusisha watu wawili na kwamba upande wa mashtaka katika shauri hilo umethibitisha kosa bila kuacha shaka.

> **Alidai mrufani alikiri kwamba Februari 11, 2022 alikuwa nyumbani kwa shahidi wa pili na alipewa kazi ya kumfanyia tiba bint**

Alidai mrufani alikiri kwamba Februari 11, 2022 alikuwa nyumbani kwa shahidi wa pili na alipewa kazi ya kumfanyia tiba binti.

Wakili Agness alidai kuwa binti katika ushahidi wake, anadai mrufani alimwagiza akachukue maji chooni, binti alikwenda na mrufani alimfuata akiwa na dawa katika maji.

Inadaiwa mrufani alimwamuru binti avue nguo ili aoge dawa, binti alivua, akamwona mrufani anatandika karatasi chini , alimwambia anamwingilie ili hedhi zake zitoke, alimwingilia na alipomaliza alimwamuru aoge.

Inadaiwa binti alikuwa akioga huku akili kwa kuonesha hakuridhia kitendo hicho, lakini alikubali kwa sababu aliambiwa anapata tiba.

Mahakama baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, ilisema kutokana na ushahidi huo, mahakama ya chini haiwezi kusema upande wa mashtaka ulithibitisha shtaka bila kuacha shaka.

Ilisema shahidi wa kwanza hakusema lolote katika ushahidi wake kuhusu kubakwa kwa madai ya kufanyiwa tiba za jadi na kwamba aliyetoa ushahidi huo ni shahidi wa tatu.

"Katika kesi za kubaka, ushahidi mzuri unapatikana kwa aliyefanyiwa kitendo hicho, lakini katika shauri hili hayo yanakosekana," alisema Jaji Luvanda.

Baada ya kusema hayo, mahakama ilitamka kwamba upande wa Jamhuri katika shauri hilo haukuthibitisha kosa bila kuacha shaka.

Mahakama iliamuru hatia na adhabu dhidi ya mrufani viondolewe na mrufani aachiwe mara moja, labda kama kuna sababu nyingine ya kumshikilia.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Mtaalamu aonya watoto kufungiwa nyumbani

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MTAALAMU wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, Davis Gisuka, ameonya wazazi wenye tabia ya kufungia watoto wao katika mageti wakiamini kutochangamana na wengine ndiyo malezi bora.

Amesema wazazi wa aina hiyo wanatakiwa kubadilika na kuachana na utaratibu huo kwa kuwa unanyima mtoto uhuru wa kujifunza.

Gisuka anayefanya kazi katika Shirika la Crossfire alisema mjini hapa juzi kuwa watoto wanatakiwa kucheza na wengine na wakirejea ikibainika kuna mambo hayaendi vizuri, ndipo mzazi achukue hatua kuwarekebisha na watakuwa wanajifunza zaidi kuliko kuwafungia na kuwafanya kuishi wakiwa goigoi mbele ya wengine.

"Kitendo cha kuwafungia ndani ya mageti kinawafanya waendelee kucheza wao kwa wao na ndugu wa nyumbani, lakini wakitoka nje kuna mambo watajifunza kutoka kwa wengine na ni muda sahihi kwao kujifunza kupitia wengine," alisema.

Gisuka alitembelea Kituo cha Malezi na Makuzi kilichoko Disunyara, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, ziara iliyoratibiwa na Taasisi ya Anjita ambayo iliwahusisha wadau mbalimbali, lengo likiwa kuhamasisha kuwapo vituo hivyo kwa watoto wenye umri wa kuanzia miaka mitatu.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Pwani, Rachel Chuwa, alisema ili kuwa na taifa bora, lazima kuwekeza kwa watoto wakiwa wadogo. Watoto wanatakiwa kulelewa vizuri ili wakue kiakili na kimwili wakiwa na maadili mema.

Rachel alisema vituo vya malezi na makuzi vinasaidia watoto kuanza kujitambua mapema na kuchangamsha akili kwa kuwa wanahitaji kufundishwa wakiwa wadogo, kipindi ambacho wanaweza kushika vitu vingi na kuhifadhi akilini.

Alielekeza wazazi wote wenye watoto wenye umri wa kuanzia miaka mitatu, wahakikishe wanawapeleka katika vituo vya malezi na makuzi na maeneo ambako hayana, wananchi wanatakiwa kuungana na kuvianzisha.

Janet Christian kutoka Taasisi ya Anjita alsiema wamekuwa wanafanya shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo kusaidia watoto wenye mahitaji maalum.

Anjita ambayo inafanya kazi na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, imeshiriki katika kufufua kituo hicho kwa kuchangia vifaa mbalimbali vikiwamo vya michezo ambavyo vinahamasisha mtoto kupenda kwenda shuleni.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Joel Mwakapala, alisema vituo hivyo vinatakiwa kuanzishwa nchi nzima na wazazi wawekeze zaidi kwa watoto wa miaka 0-8.



Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Ilala ambaye ni Mkurugenzi wa Naya Food Africa, Rehema Sanga (katikati), akitoa maelezo kuhusu bidhaa mbalimbali anazozitengeneza kwa mwananchi aliyetembelea banda lake katika maonyesho ya wajasiriamali viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# Bodi ya Stakabadhi Ghalani yalipa Bil. 270/- wakulima wa ufuta, korosho

**Na Mwandishi Wetu,** NANYUMBU

BODI ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala imetoa Sh. bilioni 274 kwa mwaka 2022/2023 kwa wakulima wanaozalisha mazao yanayouzwa kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani yakiwamo ufuta, mbaazi na korosho mkoani Mtwara.

Katika uzinduzi wa ghala la mfumo wa stakabadhi ghalani wilayani Nanyumbu, mkoani Mtwara juzi ambako Rais Samia Suluhu Hasssan alikuwa mgeni rasmi, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani, Asangye Bangu, alisema bodi kwa msimu wa kilimo 2022/23 ilisimamia uuzaji wa ufuta tani 17,000, mbaazi tani 16,000 na korosho tani 93,000 mkoani Mtwara.

"Sh. bilioni 274 zimelipwa moja kwa moja kwa wakulima. Tunaweza kuona taarifa hizi kwa sasa kwa kuwa tunatumia mfumo huu wa stakabadhi ghalani," alisema.

Bangu alibainisha kuwa bei za mazao ya ufuta na mbaazi zimekuwa zikipanda hivi karibuni huku akitoa mfano wa bei za mbaazi ambayo imependa kutoka Sh. 500 kwa kilo kabla ya mfumo wa usimamizi wa stakabadhi za ghala hadi kufikia wastani wa Sh. 2000 kwa sasa.

"Tulikuwa na changamoto katika bei ya korosho kutokana na ukweli kuwa soko halikuwa zuri, lakini tunaamini tutafanya vizuri msimu ujao," alisema.

Bangu alisema mpango wa bodi yake ni kusambaza Mfumo wa Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani nchi nzima ili kunufaisha wakulima wengi nchini.

Mratibu wa Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu nchini (TANIPAC), Clepin Josephat, akizungumza wakati wa hafla hiyo, alisema mradi huo wa sumukuvu wenye thamani ya Sh. bilioni 78.9 unafadhiliwa na Serikali ya Tanzania kwa ushirikiano na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) na utatekelezwa kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar.

"Hadi sasa tumejenga maghala 14 kwa ujumla, 12 yakiwa Tanzania Bara na mawili visiwani Zanzibar. Maghala yote yamekamilika na yako katika viwango vya juu kabisa," alisema.

Aliongeza kuwa mradi wa taasisi yake wilayani Nanyumbu umehusisha ujenzi wa ghala la taasisi hiyo ambalo limejengwa kisasa na litaendeshwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.

## RC ashtuka uchafu mazingira manispaa

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

WAKAZI wa Mji wa Singida na vitongoji vyake wako hatarini kukumbwa na magonjwa ya kuambukiza na ya mlipuko kutokana na uongozi wa manispaa hiyo kutosimamia usafi wa mazingira.

Kutokana na tishio hilo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ametoa miezi miwili kwa uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida kutunga sheria ndogo ya kusimamia usafi katika mji huo.

Serukamba alitoa maagizo hayo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Usafi Duniani iliyoadhimishwa kimkoa katika Manispaa ya Singida kwa kufanya usafi kwenye Soko la Mtaa wa Msufini, kata ya Mughanga.

Alisema kuwapo sheria hiyo kutasaidia kutoa adhabu kwa kila mwananchi atakayebainika anatupa uchafu bila kujali ni aina gani ya uchafu uliotupwa na mhusika. Adhabu pendekezwa iijumuishe faini ya Sh. 50,000.

"Tunataka watu wote wanaotupa uchafu tuwape adhabu. Ukitupa chupa ya maji tukikukamata unalipa Sh. 50,000, ukitupa karatasi tukikukamata unalipa on tukifanya hivyo, mji wetu utakuwa safi maana tumeambiana vya kutosha, tumeonyana vya kutosha. Ninadhani wakati umefika sasa tuambiane kwa adhabu," aliagiza.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa, manispaa ni chafu na wanaoichafua ni wakazi wa Mji wa Singida na walioshindwa kuwasimamia ni viongozi waliopewa dhamana ya kuwasimamia wananchi.

"Sasa leo ninakuja kutoa maelekezo na yatakuwa magumu kidogo. Unajua watu wa Singida mnajua sana kulalamika, mnajua sana kutafuta vyombo vya habari mlalamike, lakini mnalalamika bila kutekeleza wajibu wenu.

"Wajibu wa usafi, wajibu wa kuweka mazingira safi ni wajibu wa kila Mtanzania. Nchi hii inaendeshwa kwa sheria na hatuna namna, lazima tutekeleze sheria," alisisitiza.

Serukamba alitumia fursa hiyo kuutaka uongozi wa Manispaa ya Singida kuweka watendaji au watu ambao wakimkamata mtu aliyetupa uchafu, wapatiwe sehemu ya faini atakayolipa mhalifu. Watu watafanya kazi hiyo kwa uaminifu mkubwa.

"Tunataka kila mtu amkabe mwenzake. Nikikukamata umetupa chupa, ninakupeleka kwa mkurugenzi. Ukilipa Sh. 50,000, Sh. 20,000 za kwangu ya kukamata na Sh. 30,000 zinakwenda halmashauri na mkifanya hivyo, mji huu utakuwa safi na mji wetu ukiwa safi, magonjwa yatapungua," alisema.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alisema kununua magari ya kusomba taka ni jambo moja, kununua vifaa vya usafi ni jambo lingine, lakini maeneo kuwa safi ndiyo matokeo yanayotakiwa katika kila eneo.

Aliwataka wananchi kujitokeza kufanya usafi katika maeneo yao na iwe desturi yao badala ya kuendelea kuimba wimbo katika vyombo vya habari au kuyasikia kupitia midomo ya viongozi wakisisitiza usafi.

Alisema ni aibu na fedheha kubwa mpaka Mkuu wa Mkoa atoke kuingilia suala hilo ndipo wananchi wafanye usafi.

Ofisa Mazingira wa Manispaa ya Singida, Theresia John, alizitaja changamoto zinazoikabili Idara ya Mazingira ni pamoja na ushiriki mdogo wa wananchi katika usafishaji maeneo yao, uzalishaji mkubwa wa taka kutokana na ongezeko la watu na shughuli za kiuchumi kulinganisha na vitendea kazi vilivyoko.

Katika maadhimisho hayo, Serukamba pia alipiga marufuku wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, kuendelea kufanya biashara zao kwenye maeneo ya miundombinu ya barabara.

Pia aliagiza uongozi wa manispaa kutoa leseni za biashara kwa wamiliki wa nyumba watakaowakaribisha wafanyabiashara hao kuendesha shughuli zao kando ya nyumba zao.



## HABARI KASKAZINI

## Mfanyabiashara akutwa amefariki dunia kando ya reli

**Na Steven William,** MUHEZA

MMILIKI wa Taasisi ya Baruti inayojishughulisha na ukopeshaji fedha wilayani Muheza, Robert Baruti, amekutwa amefariki dunia pembeni ya reli huku akiwa na jeraha kubwa kwenye paji la uso.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Almachius Mchunguzi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa lilitokea jana asubuhi katika Mtaa wa Masuguru karibu na nyumba yake.

Alisema polisi wanaendelea na uchunguzi na kwamba mwili umehifadhiwa katika chumba cha maiti hospitali teule Muheza huku akiwataka ndugu kuwa watulivu katika kipindi hiki kigumu.

Mkuu wa Upelelezi wa Polisi wilayani Muheza, Charles Ntenga na daktari kutoka Hospitali ya Teule Muheza, Juma Mombokaleo, walifika eneo la tukio na kukuta mwili huo na kuanza kuuchunguza.

Tukio hilo lilizua hofu kwa wakazi wa eneo hilo ambao walijitokeza kwa wingi wakiulizana kilichomkuta mfanyabiashara huyo hadi kupoteza uhai wake.

Marehemu Baruti wakati wa uhai wake alikuwa mstari wa mbele kwenye Michezo na alikuwa Mwenyekiti wa Tawi la Yanga Imara wilayani Muheza.

Jana, marehemu Baruti alipelekwa Musoma kwa ajili ya mazishi.

**Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Almachius Mchunguzi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa lilitokea jana asubuhi katika Mtaa wa Masuguru karibu na nyumba yake.**

# Idadi ya watalii Hifadhi ya Taifa Saadan yazidi kupaa

**Na Hamida Kamchalla,** PANGANI

IDADI ya watalii wanaoingia nchini na kuitembelea Hifadhi ya Taifa ya Saadan, imeongezeka kutoka 3,400 hadi kufikia 29,000.

Mbali na kuongezeka kwa idadi hiyo, pia mapato yatokanayo na sekta hiyo yameongezeka kutoka Sh. milioni 40 mwaka 2005 hadi kufikia Sh. bilioni 1.6 mwaka 2023.

Katika mahojiano yake na Nipashe jana, Ofisa Utalii wa Hifadhi hiyo, Athuman Mbae, alisema hifadhi hiyo ni ya kipekee yenye uwezo wa kuvutia watalii ndani na nje ya nchi.

"Baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuzindua filamu ya The Royal Tour, inayotangaza utajiri na utalii wa vivutio na hifadhi za Tanzania, kumekuwa na mafuriko ya watalii Saadan.

"Kimsingi, bado tunaendelea kuboresha miundombinu na kuweka mazalia mapya ya viumbe ili kuhakikisha wageni wote wanaotembelea hifadhini, wanapata ladha tofauti ya vivutio vya utalii."

Alisema moja ya kivutio cha kipekee katika hifadhi hiyo katika ukanda wa Afrika Mashariki, ambacho huwezi kukipata sehemu yeyote, ni ufukwe wa Bahari ya Hindi kuungana ana kwa ana na mbuga ya wanyamapori.

Aidha, akizungumzia mafanikio hayo, Mkuu wa Wilaya ya Pangani, Zainab Abdallah, alisema tayari wameanza mchakato wa kuhamasisha uwekezaji kwenye hifadhi ya hiyo.

Uwekezaji unaohitajika ni sehemu ya kuunga mkono kampeni ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Alisema kuwa wameamua kufanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya uchumi baada ya kuona ndiyo kipaumbele cha serikali katika kuimarisha maisha ya Watanzania kiuchumi lakini pia kuhakikisha serikali inaendelea kuongeza mapato na kurahisisha maisha kwa wananchi.

Alisema: "Nataka niwahakikishie kuwa Serikali ya Pangani, tumejipanga kutangaza vivutio vya utalii tulivyo navyo lengo letu ni kuhakikisha watalii wengi wanakuja kutembelea hifadhi yetu ya Saadan na vivutio vinavyopatikana katika wilaya yetu.

"Tunatamani Watanzania wengi hasa wakazi wa Dar es Salaam kipindi cha mwisho wa juma, waje Saadan. Waje wenzetu kutoka Zanzibar, Mikoa ya Pwani na hata Kanda ya Kaskazini waje watembelee hifadhi hii."



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (wa pili kulia) na Meneja wa Mawasiliano na Uendelevu wa Serengeti Breweries Ltd, Rispa Hatibu (wa pili kushoto), Katibu Tawala wa Wilaya ya Hanang, Athaumani Likeyekei (kushoto) na Mkuu wa Wilaya hiyo, Janeth Mayanja, wakifurahia jambo wakati wa kufungua mafunzo ya "Learning for Life", mjini Hanang mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima wachachamaa kuporomoka bei ya mbaazi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

KUSHUKA kwa bei ya mbaazi kutoka Sh. 2,280 kwa kilogramu moja hadi kufikia Sh. 2,190, kumewaibua wakulima wanaounda Ushirika wa Kilimo na Masoko wa Gendi-AMCOs, kupaza sauti kuhusu kuporomoka kwa bei ya soko.

Bei hiyo ya soko kwa kilogramu moja katika Halmashauri ya Mji wa Babati mkoani Manyara, imeporomoka kwa Sh. 90, licha ya kiwango hicho kuonekana kidogo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana, baadhi ya wakulima, akiwamo Gabriel Inogas, alisema licha ya bei ya mnada wa mbaazi kushuka kidogo bado bei iliyopo sokoni wanaona itapunguza makali ya gharama za uzalishaji.

"Kwanza, tunaishukuru serikali kwa kukubali kuweka mfumo wa stakabadhi ghalani, kwa kuwa mfumo huo humnufaisha mkulima. Hatutakata tamaa, wakulima tutajitahidi kulima kwa wingi zao la mbaazi ili kuongeza pato la mkoa na taifa kwa ujumla na kuwa na sauti moja ili hapo baadaye bei ziweze kuwa nzuri zaidi," alisema Paulina Yohana.

Kwa mujibu wa Inogas, kabla ya serikali kuliwekea mazingira rafiki zao la mbaazi, kipindi cha nyuma bei zilikuwa hazieleweki na kilogramu moja ilikuwa inauzwa kwa Sh. 300.

Alisema mnada uliopita, kilogramu moja ya mbaazi ilinunuliwa kwa Sh. 2,280 ila mnada wa sasa, kilogramu moja inanunuliwa kwa Sh. 2,190 sawa na pungufu ya Sh. 90.

Akizungumzia mfumo huo, Thomas Sambu, alisema ameridhika na bei ya soko japo imeshuka kidogo.

Kaimu Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika mkoani Manyara cha Rift Valley Cooperative Union (RIVACU), Vivian George, alisema wao wanahakikisha mkulima anapeleka ghalani mzigo ambao ni safi.

George, alisema kwa mnada wa dengu walioufanya Wilaya ya Hanan'g walianza na tani 100.8, ila kwa mnada wa Halmashauri ya Mji wa Babati wakulima wamekuwa na mwamko na wamekusanya tani 254 kwenye ghala.

Akizungumzia mfumo huo mpya, Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Manyara, Absalom Cheliga, alisema mnada huo ni wa tano kufanyika kwa mkoa kutoka kwenye halmashauri tofauti.

Vilevile, alisema mfumo huo unawakutanisha wanunuzi na wakulima na wanunuzi wanatangaziwa mzigo uliopo siku moja kabla.

Alizitaja faida za mfumo huo na kuuza kwa mnada kuwa ni usahihi wa vipimo, uhakika wa malipo na kupewa bima ya mazao ili kufidia ikitokea majanga.

# Vijana 400 Hanang' kupewa mafunzo usimamizi fedha

**Na Mwandishi Wetu,** MANYARA

VIJANA zaidi ya 400 kutoka Wilaya ya Hanang', mkoani Manyara, watanufaika na programu ya 'learning for life' inayotekelezwa na Kampuni ya Serengeti Breweries Limited (SBL).

SBL inalenga kutoa ujuzi na maarifa muhimu kwa ajili ya maendeleo binafsi, ujasiriamali, usimamizi wa kifedha na mipango bora ya biashara ya nafaka.

Programu hiyo, ilizinduliwa juzi na Kampuni ya Serengeti Breweries Limited (SBL) na inatarajiwa kumalizika Septemba 21, mwaka huu.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga alisema: "Nina furaha kuona programu hii ikifanyika katika Wilaya ya Hanang. Hatua hii ni muhimu sana kwa mkoa wetu, kwa kuwa inaakisi kikamilifu lengo la Wilaya ya Hanang la kutoa huduma bora na zilizo endelevu ifikapo mwaka 2025.

"Hatua hii haitawawezesha tu vijana wetu, bali pia itachangia ukuaji wa kiuchumi na maendeleo ya Wilaya ya Hanang. Itaunda kundi la watu wenye ujuzi na uwezo wa kuleta mabadiliko chanya na uvumbuzi katika jamii yetu," alisema.


Alisema kuwa Tanzania, inajivunia idadi kubwa ya vijana, ambapo asilimia 64 ya Watanzania ni vijana, lakini tatizo kubwa la ukosefu wa ajira kwa vijana linaendelea kuwa tatizo.

"Upatikanaji mdogo wa mafunzo bora ya ujuzi unachangia tatizo hili, haswa katika Wilaya ya Hanang, ambapo vijana wanafanya karibu asilimia 70 ya idadi ya watu. Ni muhimu kutatua changamoto hii kwa dhati," alisema.

Aliongeza kuwa Programu ya learning for life, inatoa nafasi ya kuwawezesha vijana kujiajiri na kujenga ajira. Lengo kuu la SBL ni kuwasaidia kutambua fursa na kuzitumia kwa ufanisi.

"Fursa hii inawawezesha vijana kutengeneza mtandao wa kijamii, kujifunza kutoka kwa wataalamu na kupata ufahamu wa vitendo katika sekta mbalimbali, yote haya yakiwa na lengo la kupunguza ukosefu wa ajira, kupunguza umaskini na kutengeneza fursa kwa vijana wa Wilaya ya Hanang," alisema.

Kwa mujibu wa Meneja wa Mawasiliano na Uendelevu wa SBL, Rispa Hatibu, SBL inaamini kuwa kuwekeza kwa vijana ni kulinda mustakabali wa jamii.



# Fedha za TASAF zawaokoa wajawazito kujifungulia njiani

**Na Gwamaka Alipipi**

WAKAZI wa Kijiji cha Ishololo wilayani Bukombe mkoani Geita wameondokana na tatizo la kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za afya baada ya Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kutoa Sh.milioni 102 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati katika kijiji chao.

Wakizugumza na Nipashe baada ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, kutembelea ujenzi wa zahanati hiyo baadhi ya wananchi walisema kukosekana kwa zahanati kunasababisha wajawazito kujifungulia njiani.

Mele Doto alisema kituo wanachotegemea kinamama kujifungulia kipo umbali wa zaidi ya km 15 kutoka kijijini hapo.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, akishiriki kutengeneza mlango alipofanya ziara ya kukagua na kuweka jiwe la msingi katika ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Ngilimba, Kata ya Ulowa, Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama juzi. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita. **PICHA: MARCO MADUHU**

"Ukiwa na mgonjwa unalazimika kumpeleka Hospitali ya Wilaya iko Ushirombo labda utumie baiskeli na mwenye uwezo atapanda bodaboda ambazo mchana ni Sh. 5,000 lakini ukiugua usiku ni Sh.10,000 kwa hali ya huku kijijini sio rahisi mtu amudu anaona bora ajifungulie nyumbani na wagonjwa wengine wanatumia dawa za kienyeji," alisema Mele.

Mradi wa zahanati umejengwa kwa zaidi ya Sh.milioni 102 na itawahudumia wananchi zaidi ya 650 wa kijiji hicho.

Waziri Simbachawene pia alitembelea mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi ya walimu pamoja na matundu ya vyoo vilivyojengwa katika Kitongoji cha Ihulike kwa Sh.milioni 76.1.

Wakizungumzia mafanikio ya Mpango wa TASAF wananchi wa eneo hilo walisema madarasa hayo yatapunguza msongamano wa wanafunzi darasani na kwamba mbali na hiyo walengwa wamefanikiwa kupata kipato cha kuwasaidia watoto wao kielimu kwa kuwanunulia vifaa vya shule.

## Utaratibu mpya mikopo asilimia 10 wawakosha wananchi

**Na Alex Sayi,** MASWA

BAADHI ya wanufaika wa mikopo ya asilimia 10 walayani Maswa wamefurahishwa na utaratibu mpya wa utolewaji wa mikopo hiyo kupitia benki mbalimbali nchini.

Wamesema hali hiyo itapunguza urasimu na upotevu wa fedha ambao umekuwa ukijitokeza kila mwaka.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wanufaika hao akiwamo Ng'walu Ndama ambaye ni mjasiriamali alisema anaishukuru serikali kwa kuja na utaratibu huo.

Alisema awali walishindwa kuchukua mikopo kutokana na mchakato wake kuwa na masharti mengi.

Godfrey Amani ambaye ni dereva bodaboda alisema ukopaji wa fedha kwa utaratibu wa kuchukulia benki utakuwa mzuri tofauti na ilivyokuwa hapo awali, kwamba itakuwa ni ruksa kukopa hata kwa mtu mmoja mmoja na kudhibiti utaratibu wa baadhi ya watu kwenye vikundi kuhodhi fedha hizo.

Mwenyekiti wa UWT Taifa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa CCM, Mery Chatanda, akizungumza mwanzoni mwa wiki katika mkutano wa hadhara wilayani Maswa alieleza serikali imeshaweka utaratibu wa utolewaji wa mikopo hiyo kwamba ianze kutolewa na benki.

Alieleza kuwa tayari kamati maalumu iliyoundwa kutekeleza jambo hilo imeshakamilisha utaratibu wa namna ya kuendelea na utoaji wa mikopo hiyo na Bunge litapewa taarifa hiyo.

"Serikali ina nia ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa sasa mikopo hii itatolewa na benki na mikopo hii haina masharti ya kukopa, kivikundi hata mtu mmoja atawezа kukopa na utakapokamilisha kujaza fomu katika ofisi za maendeleo ya jamii," alisema Chatanda.

## Wakulima wa korosho Ushetu kupewa tani 3 za miche

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Ushetu mkoani Shinyanga inatarajia kutoa tani tatu za miche ya korosho katika msimu wa kilimo wa mwaka 2023/24 kwa wakulima.

Lengo kuu likiwa ni kuhakikisha wakulima wanajielekeza katika kulima mazao ya chakula na biashara ili kukabiliana na baa la njaa.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri hiyo, Mapenzi Mshana, aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe na kueleza kuwa kilimo hicho kilianza tangu mwaka 2019.

Alisema mpaka sasa wameweza kugawa miche ya zao hilo kwa wakulima na madiwani.

Halmashauri hiyo inategemea mapato yake kwa kiwango kikubwa katika tumbaku, pamba, alizeti, mahindi, mpunga, viazi vitamu na karanga na sehemu ndogo katika mgodi wa dhahabu Mwabomba uliopo Kata ya Mwabomba hali iliyowafanya kuhamasisha kilimo hicho ili kuongeza vyanzo vya mapato.

Alisema, kila mwaka wamekuwa wakinunua miche ya zao hilo na kuzigawa kwa wakulima na mwaka jana waligawa miche zaidi ya 12,000.

Mshana alisema kwa mwaka huu wanatarajia kununua miche zaidi ya tani tatu na kuzigawa kwa wakulima na taasisi mbalimbali ikiwamo shule za msingi, sekondari na madhehebu ya dini yenye maeneo ya kilimo.

"Miche hii tunainunua Mtwara na kuileta hapa Ushetu na mche mmoja tunaununua kwa Sh.5,000 na lengo letu ni kuhakikisha kilimo hiki kinalimwa sana kama yalivyo mazao mengine ya biashara, tunatarajia kununua mashine ya kubangua korosho kama walivyofanya Halmashauri ya Ikungi mkoani Sindia," alisema Mshana. Alisema kuna baadhi ya wakulima wamevuna sehemu ya korosho na wamehifahi ndani isipokuwa soko limekuwa tatizo.

Mshana alisema tatizo kubwa wanalokutana nalo ni upatikanaji wa dawa ya kupulizia ili kupambana na ukungu katika majani ya korosho.

# RC Makalla apokea kero kibao za wananchi, asikitika

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla amekutana na wananchi na kupokea malalamiko mengi yanayowasibu ikiwamo baadhi ya viongozi na watumishi wa serikali kuwa chanzo cha migogoro mkoani hapa.

Mkutano huo uliofanyika juzi ofisini kwake, ulihudhuriwa na wakuu wa wilaya, wakurugenzi pamoja na viongozi wa idara mbalimbali kutoka halmashauri zote za mkoa.

Mkutano huo ulipewa jina la 'Ongea live na Mkuu wa Mkoa' ambako baadhi ya wananchi walitaja chanzo cha kero zao kutokutatuliwa ni urasimu wa baada ya viongozi waliopewa majukumu ya kusimamia sekta husika.

Mmoja wa wananchi hao, Zakayo Karebo alieleza kuwa mwaka 2021 alikuwa na mpango wa kujenga kituo cha mafuta na kufuata utaratibu kwa kufuatilia vibali kutoka EWURA na NEMC ambako alilipia Sh. milioni 400.1 kwa ajili ya ukaguzi wa kimazingira na kuruhusiwa kuendelea na utekelezaji wake.

Kadhalika alitaja kutumia gharama ya Sh.milioni 480 kununua viwanja vya majirani zake wawili baada ya kutakiwa kuongeza ukubwa wa eneo na kuelezwa kuwa halifai kwa ujenzi wa kituo cha mafuta kutokana na kuwa dogo.

Alieleza kuwa licha ya kufuata taratibu zote alitakiwa kupata kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza ili aendelee na utekelezaji wa mradi wake lakini ni zaidi ya miaka mitatu hajapatiwa kibali hicho, hali inayomkatisha tamaa kuendelea na mradi wake.

"Sheria za ujenzi wa vituo ni kupishana kwa mita 200 na eneo nilipohitaji kufanya ujenzi huo kuna urefu wa zaidi ya mita hizo lakini licha ya kufuata taratibu hizo bado mkurugenzi ameshindwa kuniruhusu kuendelea na ujenzi," alisema na kuongeza:

"Vilevile nilimwandikia barua kupata mrejesho wangu sikujibiwa nikaamua kwenda kwa Katibu Tawala Mkoa nikakabidhi barua yangu ya hatua nilizopitia vilevile haikujibiwa," alieleza Karebo.

Kwa mujibu wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza walieleza kuwa kusitishwa kwa ujenzi wa kituo hicho ni maelekezo za ya Kamati ya Usalama ya Wilaya kuwa katika eneo hilo vituo ni vingi hali inayohatarisha usalama wa wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, alikana juu ya kamati yake ya usalama kuhusika katika kuzuia ujenzi huo na kueleza kuwa wao waliishauri idara husika kuangalia utaratibu wa utolewaji wa vibali katika ukanda huo, kutokana na kuwapo kwa kiasi kikubwa ya vituo vya mafuta.

Baada ya kikao hicho, Makalla alisikitishwa na hali wanazopitia wananchi hao kwa kuzungushwa mara kadhaa.

"NEMC, EWURA na kamati ya madiwani wameridhia kituo kijengwe na mtu tayari kawekeza hela zake kwani kosa ni la kwake au ni letu sisi. Naomba nipate nyaraka zake mimi na kamati yangu tutafika kwenye eneo hilo na kulipatia ufumbuzi," alieleza Makalla.

Pia aliwaagiza wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri pamoja na wakuu wa idara kuhakikisha wanatatua migogoro sugu ya ardhi kwa kuwafikia wananchi katika maeneo yao, huku akiahidi kuendelea na utaratibu aliouita wilaya hadi wilaya.




Ukurasa 12

**WAPINZANI katika meza ya TCD...**
**Wanapokuwa sauti moja tume huru, kushuka kwa demokrasia**



Ukurasa 13

MEYA YAGI KIARATU
Mwanamama anayepambana kila leo kuibadilisha Singida



Ukurasa 14

**KITABU CHAKE MBIONI KUZINDULIWA...**
**Dk. Salim Ahmed Salim: Hazina ya Afrika aliyepewa ubalozi miaka 22**


# siasa

JUMATANO SEPTEMBA 20, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


MGOMBEA BINAFSI ASUBIRI

# Wasira amshtukia akihisi muuza unga, jambazi aweza kutinga ikulu

## •Ahofia nchi kutumbukia nyongo akihimiza ufanyike utafiti kwanza

**Na Sabato Kasika**

MATAMANIO ya kuwapo kwa mfumo unaoruhusu mgombea binafsi, ni miongoni mwa mambo ambayo yaliteka mjadala katika mkutano wa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Demokrasia.

Jukwaa hilo la wanasiasa likifanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni na kushirikisha wadau mbalimbali, wakiwamo wanasiasa na asasi za kiraia, linasikia sauti ya mbobezi na guru la kisiasa, Stephen Wasira, akionyesha kukosa imani na kuwapo mgombea huru asiyetokana na chama cha siasa.

Katika mjadala huo, Wasira anasema ni vyema kabla ya kuruhusu kuwapo mgombea huyo, kwanza ufanyike utafiti ili kujua mafanikio yaliyopatikana katika nchi zilizoruhusu mfumo huo.

"Bila kufanya utafiti, tunaweza kujikuta tukikabidhi nchi kwa muuzaji wa dawa za kulevya na kuingia katika matatizo, hivyo ni vyema utafiti ufanyike ili kujua kujiridhisha," anasema.

Anafafanua kuwa uchaguzi unatumia fedha nyingi, na kwamba anayetaka kuwa mgombea binafsi ni muhimu kujua vyanzo vyake vya mapato ili kuepuka wauzaji wa dawa za kulevya wanaoweza kuharibu.

"Kabla ya kuendelea nifafanue kuwa ninatoa maoni yangu si ya chama. Ndugu zangu tunapojadili suala la mgombea huyu asiyetokana na chama cha siasa ni vyema tuwe makini, ndio maana nikasema utafiti ufanyike kwanza si kwamba ninapinga bali tusijikute tunaweka nchi katika matatizo," anasisitiza.



Stephen Wasira akizungumza kwenye mkutano wa Siku ya Demokrasia Duniani. **PICHA: SABATO KASIKA**

Kauli ya Wasira inakuja baada ya waandaji wa mkutano huo, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kuzindua kitabu chao kiitwacho, miaka 30 ya Demokrasia ya Vyama Vingi nchini Tanzania 1992 mpaka 2022. Tafakari ya Maendeleo, Changamoto na Fursa.

Kitabu hicho kinaelezea kupanda na kushuka kwa vyama vya siasa, jinsi kituo hicho kilivyoshiriki kufanikisha kesi uwapo wa mgombea huru ingawa hadi sasa serikali haijaruhusu.

### KILIO CHA WADAU

Mkurugenzi Mtendaji Mstaafu wa LHRC, Dk. Hellen Kijo-Bisimba, ndiye anayefungua pazia kilio cha mgombea huru huku akifafanua kuwa jambo hilo halikwepeki, ni muhimu kwa ustawi wa demokrasia.

"Ndani ya vyama vya siasa kuna changamoto nyingi zikiwamo ambazo zinakwamisha baadhi ya watu wenye nia ya kuongoza, hao wangeachwa wawe huru kugombea," anasema Dk. Hellen.

Anaongeza kuwa miaka 30 ya mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini, suala la mgombea binafsi ingawa lilitolewa hukumu baada ya kesi ya Mchungaji Christopher Mtikila (marehemu), limewekwa kapuni.

Mwanaharakati huyo anaungwa mkono na Katibu wa Baraza Kuu la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) (BAWACHA), Catherine Ruge, kwamba kuna wanawake si wanachama wa vyama vya siasa wanaotaka kuongoza, lakini wanakwama.

"Wanakwama kutokana na mfumo wa sasa wa kupitia katika vyama, ninadhani kuna haja ya kuwaacha Watanzania wawe huru kuchagua viongozi wasiotokana na vyama," anasema Catherine.

Mchambuzi wa siasa, Deus Kibamba, anasema suala hilo limecheleweshwa kwa muda mrefu, na kwamba ni vyema Watanzania wakaruhusiwa kuwa huru kuwania uongozi bila kupitia kwenye vyama.

Baada ya maoni hayo ndipo Wasira anaibuka na kutoa angalizo na kuwataka wanasiasa, wanaharakati, wachambuzi wa siasa na wadau wengine nchini kuwa makini kwenye suala hilo la mgombea binafsi.

Mkazo wake ni kutaka ufanyike utafiti kwanza, ili kujiridhisha kama mfumo huo una manufaa kwa maslahi ya taifa na si kwa wagombea, ndipo hatua zichukuliwe.

Kwa mujibu wa katiba, mgombea lazima awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, awe na umri wa kuanzia miaka 50, awe na sifa ya kuwa mbunge.

Vilevile awe na shahada inayotolewa na chuo kinachotambuliwa kisheria, hajawahi kufungwa jela. Kwa maana hiyo, mgombea binafsi atawajibika kuwa na sifa kama hizo, hivyo ni maamuzi ya Watanzania rais wanayemtaka atokane na chama au awe huru na si vinginevyo.

### KATIBA MPYA

Mwenyekiti wa Baraza la Vijana CHADEMA (BAVICHA), John Pambalu, anasema katika miaka 30 ya mfumo wa vyama vingi, nchi imeshindwa kuandika kati-

INAENDELEA UK. 14

WAPINZANI KATIKA MEZA YA TCD...

# Wanapokuwa sauti moja tume huru, kushuka kwa demokrasia



Mwenyekiti wa TCD, Profesa Ibrahim Lipumba (katikati), akiongoza Jukwaa la Hali ya Demokrasia nchini. **PICHA: HALFANI CHUSI**

**Na Halfani Chusi**

KILIO cha muda mrefu cha vyama vya upinzani kuhitaji tume huru ya uchaguzi, uhuru wa kujieleza na kushuka kwa demokrasia bado kinaendelea.

Wadau hao wanapokutana kwenye jukwaa la Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), kwa pamoja wanafikisha kilio chao serikalini.

Anayefungua pazi la kutuma ujumbe ni Mwenyekiti wa Chama cha Umma (CHAUMA), Hashim Rungwe, anayesema demokrasia imeshuka kwa sababu vyombo vya dola vimekuwa vikiingilia mazungumzo ya watu hasa yanayohusu siasa na wakati mwingine kuyatibua.

Anagusia suala la wanasiasa kuishi bila uhuru, iwe nyumbani, mtaani na popote kila siku, kwa sababu yakufuatiliwa na polisi.

Makamu Mwenyekiti wa NCCR Mageuzi, Joseph Selesini, anasema demokrasia imeshuka kwa sababu uchaguzi unasimamiwa na upande mmoja, hakuna tume huru ya uchaguzi, utaratibu unaotumika kumpata mgombea ni kama wa mchezaji na mwamuzi.

"Uchaguzi wa serikali za mitaa, unasimamiwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), hii ni shida kwa sababu huko wamejaa viongozi wengi wa CCM unadhani watakubali kiongozi wa upinzani apite?

"Tunataka usimamiwe na tume huru ya uchaguzi, tunateswa, tunapigwa na polisi wanatunyanyaswa ndiyo maana kila siku demokrasia inazidi kudidimia.

"Ukifika wakati wa uchaguzi chama tawala kinapewa mabilioni, lakini vingine havipati hata shilingi vinashindwa kufanya hata mikutano ya kisiasa hili haliko sawa," analalamika Selasini.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Maftaha Nachuma, anaendeleza kilio kwamba hali ya demokrasia na uhuru wa kujieleza upo pabaya.

Anatetea hoja yake kwamba, vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo kazi yao ni kulinda usalama wa raia na mali zao, vinatibua uchaguzi uliowekwa na sheria.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, anasema kama taifa linataka demokrasia na uhuru wa kujieleza tiba ni katiba mpya.

Anakumbushia kuwa mapema mwaka huu Rais Samia Suluhu Hassan, alizindua kamati ya kuendeleza mchakato wa katiba mpya lakini mpaka sasa hakuna kilichoendelea jambo linalomtia mashaka.

"Kwa sasa kuna kitu cha ajabu, kuna uhuru wa kujieleza lakini hakuna uhuru baada ya kutoa maelezo mfano mzuri ni wale ndugu zetu wanaopinga mkataba wa bandari walikamatwa na kupewa kesi ya uhaini," anadai Mnyika.

Juma Duni Haji, Mwenyekiti wa ACT- Wazalendo, hayuko mbali na watangulizi wake anasisitiza iundwe tume huru ya uchaguzi kabla ya mwaka 2023 ili uchaguzi wa serikali za mitaa wa 2024 na mkuu wa 2025 uwe huru, haki, kuaminika na kukubalika.

Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania, Profesa Ibrahim Lipumba, anasema tangu mfumo wa vyama vingi ulipoanza haujafanikiwa kujenga demokrasia ya kweli akibainisha kuwa kuna matukio mengi yanayodhihirisha hayo.

"Katika uchaguzi wa mwaka 1995, wabunge wa vyama vya upinzani walipata asilimia 45 katika idadi ya wabunge 232, CCM walikuwa 186 upinzani walikuwa 46, lakini katika uchaguzi wa 2015 vyama vya upinzani vilipata wabunge 68 kati ya wabunge 257.

"Uchaguzi wa 2020 upinzani uliambulia wabunge wanane pekee kati ya 264, tangu tumeanza uchaguzi Kilimanjaro ilikuwa inatoa wabunge wapinzani lakini mwaka huo hakuwapo hata mmoja.Ni wazi, hii ilikuwa sunami ya uchaguzi na hili jina la sunami alilitoa mtani wangu mstaafu Jakaya Kikwete ndiye aliyesema kwa mara ya kwanza kwamba matokeo hayo ni sunami ya uchaguzi," anakumbusha Lipumba, ambaye ni Mwenyekiti wa CUF.

Anaongeza kuwa hali hiyo si njema, inaonyesha hakuna demokrasia ingawa alipoingia Rais Samia angalau kauli zake zinaleta matumaini anaposisitiza "nchi ni yetu sote".

**CCM YAJIBU**

Ni hoja, ambazo zilihitaji majibu na Makamu Mwenyekiti CCM Bara, Kinana anatoa maelezo, akikiri kuwapo upungufu na kutekeleza katika kusimamia sheria, akijitetea kwamba uhuru wa kujieleza na demokrasia vipo.

Japo ana angalizo lake kwamba watu wanavuka mipaka na kuvunja sheria za nchi ila kuna kasoro katika utekelezaji wake pale wanapopitiliza hasa namna ya kuwadhibiti.

"Tangu Rais Samia ameingia madarakani juhudi zimefanyika, mtakumbuka alipopokea tu kijiti alianza kuongelea mchakato wa katiba mpya akija na mkakati wa kugusa maeneo matatu ya tume huru ya uchaguzi, uchaguzi wenyewe pamoja na namna vyama vya siasa vitakavyosimamia uchaguzi," anafafanua Kinana.

**MAAZIMIO**

Vyama vya siasa viliazimia mengi ikiwa ni pamoja na vyama vya siasa Zanzibar, viendeleze utashi wa kisiasa katika utekelezaji wa kudumisha dhana ya maridhiano, kuelekea uchaguzi mkuu 2025, uchaguzi wa Zanzibar ufanyike siku moja.

Aidha, serikali iwezeshe na kusaidia majadiliano baina ya vyama vya siasa, asasi za kiraia na mashirika ya kiserikali ili kuhakikisha kunakuwa na mtazamo wa pamoja katika kujenga dhana ya ushirikiano kushinda kwa hoja bila kupingwa.

Maazimio mengine ni kuwekeza uhuru wa kutoa maoni na kujieleza kwa wananchi, viongozi vyama vya siasa na asasi za kiraia, vyama vya siasa viwe na kanuni zinazoelezea na kuongoza mchakato wa uteuzi wa wagombea wa nafasi za viti maalumu vya wanawake zinazoakisi misingi ya uwazi, usawa na demokrasia.

Fedha zilizotengwa na serikali kugharamia elimu ya katiba ya mwaka 1977 zipelekwe kwa asasi za kiraia na elimu hiyo iwe endelevu.

Aidha, muswada wa mabadiliko ya katiba upelekwe pamoja na wa tume huru ya uchaguzi bunge lijalo kama ilivyofanyika mwaka 1992 wakati wa kurudisha vyama vingi.

Muda uliobakia kuelekea uchaguzi ni mfupi, mkutano wa kitaifa wa maridhiano uliofanyika April 2022 Dodoma ulijadili na kuwasilisha serikalini muswada wa mfumo sheria ya uchaguzi huru na wa haki.

> "Tunataka usimamiwe na tume huru ya uchaguzi, tunateswa, tunapigwa na polisi wanatunyanyaswa ndiyo maana kila siku demokrasia inazidi kudidimia.

> "Kwa sasa kuna kitu cha ajabu, kuna uhuru wa kujieleza lakini hakuna uhuru baada ya kutoa maelezo mfano mzuri ni wale ndugu zetu wanaopinga mkataba wa bandari walikamatwa na kupewa kesi ya uhaini," anadai Mnyika.

MEYA YAGI KIARATU

# Mwanamama anayepambana kila leo kuibadilisha Singida

**Na Claudia Kayombo, SINGIDA**

NI mwanamke anayeufahamu kikamilifu mkoa wa Singida na kukielewa kwa kina kile achotaka kukizungumzia, ni Yagi Kiaratu, mwanamama Meya wa Manispaa ya Singida ambaye huona fahari kuelezea mazuri na hata changamoto za mkoa wake mbele ya yeyote.

Mama huyo diwani wa kata ya Majengo, mjini hapa, anayesema wakati anaingia madarakani 2015, barabara zote kwenye kata yake hazikuwekwa lami, lakini sasa ana mengi ya kujivunia.

"Nikiwa mwakilishi wa kata hii, kupitia mradi wa Benki ya Dunia (WB), tumeshirikiana na viongozi wenzangu kusimamia barabara zote kuu za kata ya Majengo na sasa zina lami, pia zipo taa," anasema.

Anafafanua kuwa taa hizo zimetoa na kuongeza fursa za kiuchumi kwa wafanyabiashara hususan kinamama kufanya biashara zao ndogondogo hadi usiku huku wakiwa na uhakika wa usalama wao.

"Pia uongozi wake umemaliza tatizo la uhaba wa maji Sekondari Mwenge yenye wanafunzi zaidi ya 1,000 na ile ya msingi Ukombozi yenye wanafunzi zaidi ya 1,800."

Yagi anasisitiza kuwa mbunifu katika uongozi akieleza kuwa wamejitahidi kutafuta wahisani kumaliza tatizo la maji katika shule mbili hizo.

Anabainisha kuwa mchakato unaofanyika sasa ni kuhakikisha mabomba yanasambazwa katika kila kona ya Shule ya Ukombozi ili kuwawezesha wanafunzi kupata maji ya kunywa na kusafishia mazingira eneo lolote shuleni hapo.

Anaeleza kuwa hakuna tatizo la wanafunzi kukaa sakafuni kwa sasa kwa kukosa madawati baada ya juhudi za kukarabati madarasa chakavu katika Shule ya Ukombozi, tumenunua madawati ya kutosha.

Aidh, anasema pia hivi karibuni wamekubaliana kujenga uzio katika shule hiyo ya msingi, ujenzi unatarajia kuanza wakati wowote ambao ukikamilika utaleta uhakika wa usalama kwa wanafunzi na walimu wao.

"Naishukuru serikali imeleta fedha tunaendelea kujenga madarasa na kukarabati yale yaliyochakaa. Rai yangu kwa serikali yetu sikivu ni kuomba tujenge ghorofa, kwa sababu nafasi katika shule nyingi ni finyu, ningependa kuona mfano Ukombozi, madarasa ya ghorofa," anashauri Meya.

**UZALISHAJI ALIZETI**

Yagi anazungumzia kilimo cha alizeti, akasema baada ya mlipuko wa UVIKO-19, uzalishaji wa mbegu za mafuta ulikuwa mdogo nchini, hivyo serikali iliweka mkakati wa kuzalisha mbegu za mafuta ikiwamo alizeti na michikichi ili taifa liondokane na tatizo la uhaba wa mafuta.

Anasema katika kutekeleza mkakati huo uliozinduliwa na Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, mwaka huu, wakulima wamepata mazao mengi lakini sasa wanalalamikia bei ndogo ya mazao yao. Hata hivyo hakutaja bei ya alizeti sokoni hapo.

Anazungumzia masoko akieleza kuwa lipo soko kuu na soko la mkoa na la vitunguu, nia ni kuyakarabati yawe katika hali nzuri na kupitia mapato ya ndani manispaa hiyo itazidi kuyaimarisha yale madogo.



Meya Yagi Kiaratu. **PICHA: CLAUDIA KAYOMBO**

Meya Yagi anagusia suala la machinjio kuwa katikati ya mji, akisema ilikuwa inahatarisha usalama wa watu waliokuwa wanaizunguka, hivyo wanaijenga nyingine kwa gharama ya milioni 120 eneo la Naida barabara ya kwenda Dodoma, ambayo ipo katika hatua za mwisho na kwamba itaanza kutumika wakati wowote kuanzia sasa.

Akizungumzia kuhusu usafi wa mazingira, anasema kwa siku halmashauri ya manispaa hii inazalisha taka ngumu tani 120, ambazo zilikuwa zinamwagwa dampo kuu, lililokuwa pembeni ya barabara ya Mwanza, sasa limehamishiwa eneo jingine kupisha mradi wa kiuchumi eneo hilo.

Anafafanua kuwa taka hizo zilikuwa zinachukuliwa kutoka maeneo zinakozalishwa badala ya kuzihifadhi katika madampo ambayo yalikuwa yanaongeza uchafu.

"Kupitia mapato ya ndani tumenunua magari mawili mapya ya kuzolea taka yenye thamani ya Shiling milioni 220. Katika masuala ya kiutawala, tumeyaboresha, mfano mgambo wa halmashauri wanavaa sare tofauti na wengine ili kuwatofautisha," anasema.

Meya anazungumzia miradi inayoiongezea pato halmashauri akisema kuna mradi wa tofali imara kama zenye viwango na wameanza kuzitumia katika miradi mbalimbali wakimaliza watauza kwa mteja yeyote.

Anasema wataongeza mapato kwa kuimarisha fukwe za maziwa madogo matatu ambayo ni fahari ya mkoa huu, ili kuvutia wawekezaji katika sekta ya utalii.

"Singida tunajivunia maziwa mengi, niseme maziwa haya ni fahari ya mkoa yana historia pia, kwa mfano Ziwa Kindai na Monangi ambayo yametenganishwa na barabara, kila baada ya miaka kadhaa, mvua zinapoongezeka, yanaungana, mfano mwaka juzi yaliungana yakaleta adha kwenye mawasiliano."

"Lakini niishukuru serikali ilileta fedha nyingi iliyotumika kujenga barabara za juu ambazo ni utalii tosha, pia imejenga madaraja ya kupitisha maji, maji yakijaa hayawezi kuleta usumbufu kwa watu kilichobaki ni sisi kupandisha fukwe, kupanda miti na kujenga vibanda vya kupumzikia, hiyo ipo kwenye mipango yetu."

Kwa upande wa Kindai anasema wameshaanza kutengeneza barabara zinaitwa utalii road, ukienda upande wa juu wa Kindai zipo yote haya yanafanywa ili wawekezaji wavutike kuja kujenga mji wa kitalii.

Meya Yagi anaongeza pia kuwa wameingia mkataba na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, wamekubali kusaidia utunzaji wa maziwa haya ya Monangi na Kindai na wameshapeleka mihtasari wanasubiri utekelezaji wao.

Nishati ya umeme ni ajenda ya mwanasiasa huyo akisema wanakaribisha wawekezaji waje kuwekeza katika umeme wa jua na upepo.

Anawakumbusha kinamama kuwa uchaguzi wa serikali za mitaa unakaribia na kuzungumzia dhana ya mfumo dume akiwatia moyo wanawake kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwa kuwa wakipewa uongozi wanaweza, kinachotakiwa ni wajiamini.

Anasema amekuwa diwani wa Majengo katika kipindi cha mihula miwili na kwamba pamoja na wanawake wengine wameonesha uongozi thabiti kila wanapopewa nafasi na hata uzoefu unathibitisha kuwa viongozi wanaotumbuliwa ni kutokana na kutozingatia maadili ya kazi na wanaume ni wengi zaidi.

"Niwatie moyo wanawake kuwa Mungu ametupa nafasi kubwa ya kuonesha uwezo wetu, katupa uwezo mkubwa wa kubeba mambo mengi kwa wakati mmoja ndani ya familia zetu, hivyo hatuwezi kushindwa kuongoza tukipata nafasi, tujitokeze kugombea kwenye uchaguzi na fursa mbalimbali za uongozi pale zinapotangazwa," anasema Yagi.

KITABU CHAKE MBIONI KUZINDULIWA...

# Dk. Salim Ahmed Salim: Hazina ya Afrika aliyepewa ubalozi miaka 22

## • Miaka 39; akatikisa kinyang'anyiro Katibu Mkuu UN

**Na Peter Orwa**

SIKU chache baadaye mwezi huu kunazinduliwa kitabu chenye thamani kubwa katika historia na wasifu wa Watanzania na maisha yao. Hiyo ni mahsusi ikimgusa mtu muhimu na maarufu duniani, Dk. Salim Ahmed Salim.

Kwa tuliokuwapo kizazi cha zama hizo kwa umri tofauti, kwetu tuliokuwa 'mabwana wadogo' mwaka 1981 kipindi cha mpito elimu ya msingi na sekondari, tuna kumbukumbu kubwa ya jina Dk. Salim lilivyotikisa dunia, redioni na magazetini kwa mambo makuu mawili.

Ni mchapo uliotutia hamasa siku nyingi nyuma kwamba aliingia katika jukumu la ubalozi umri mdogo sana, sawa walivyo dada na kaka zetu waliomaliza shule kidato cha nne, wakati huo watu wakimaliza shule kwa umri mkubwa.

Kikubwa kilichowateka hata wazazi kipya, ni mchapo wa mwanzoni mwa mwaka huo, tukisikia na kufuatilia anavyotikisa mataifa yaliyoendelea kwenye ushindani wa kumpata Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Hapo nao wazazi na walimu wakatujazia ufafanuzi na maelezo ya ziada, maana hakukuwapo tovuti wala mitandao, simu za mkononi na kompyuta mitaani kama ilivyo sasa, lakini umoja wa jamii mitaani ulikuwa wa hali ya juu unatosha kurekebisha na tunafuatilia kwa karibu Rais Mwalimu Nyerere 'anachombeza' nini?

Dk. Salim akichuana dhidi ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa wakati huo, Mjerumani, Dk. Kurt Josef Waldheim, wakitoka sawa katika mzunguko wa kura kadhaa.

Mzunguko wa mwisho tukaripotiwa Dk. Salim 'kambwaga' (usemi wa wakati huo) kwa kura moja, kabla ya kudhibitiwa kwa kura ya veto kutoka kwa walio mpinga, kabla nafasi hiyo kumuliwa kupewa mtu tofauti nje ya ushindani huo.

Bado ninakumbuka umma tulivyohamasika mithiili ya watu sasa wanavyowehuka mitaani na matokeo ya mechi za soka kumshangilia Dk. Salim.



Balozi Dk. Salim Ahmed Salim, katika zama za ujana. **PICHA: MAKTABA**

Baadaye tukasikia imelazimika wote kukaa kando akapatikana mwingine kabisa, Javier Pérez de Cuéllar. Naam! Tulipokea kwa masikitiko, katika hamasa ileile ya soka, huku tukimpa saluti Dk. Salim wetu!

Leo hii mstaafu huyo Mtanzania anapotathminiwa kihistoria, namuona ana sura kuu nne, hata ikamwezesha awabebesha sifa Watanzania kwa ujumla, kwani kila alichotenda ilibaki ishara na kofia ya nchi.

Hilo linaanza na majukumu ya kitaifa yungali kijana mdogo, sambamba na hatua ya kuwahi kuwania nafasi Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Vilevile, Dk. Salim akawa Katibu Mkuu wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU); akiwa mahali hapo ana historia ya kupanda mbegu nyingi za utendaji Afrika, ikibaki kuwa kanuni ni miongozo ya kidiplomasia barani.

Leo hii kitabu alichotungiwa 'Salim Ahmed Salim: Son of Africa', kinampa wasifu kuwa mtoto Afrika, anayebakia historia ya uzalendo wa kuipigania bara na taifa lake Tanzania, kwa nafasi ya kipekee.

Nyayo kuu anazoacha sasa, anatajwa kujihusisha kuipigania Afrika huru; iliyoshikamana; imeneemeka ndani ya lindi la amani; hata inakuwa hamasa kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Mzizi wa maisha yanayoambatana na ushupavu wa Dk. Salim, sasa ina miongo mingi zaidi ya saba, kuanzia Januari mwaka 1942, alipozaliwa kwao Unguja, Zanzibar.

Hata pale akiwa kijana mdogo masomoni kwao visiwani, akawa tayari kishajitokeza kwenye siasa akibeba sura ya uongozi, mwasisi na Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wanafunzi Zanzibar uliokuwa wa kwanza kuundwa.

### RASMI KATIKA DIPLOMASIA

Akiwa amemaliza masomo katika umri mdogo, ikiwa ndio kwanza Muungano wa Tanganyika na Unguja unapatikana mwaka 1964, Dk. Salim akiwa na miaka 22, akawa ameaminika kwenye siasa za Muungano, akateuliwa na Rais Julius Nyerere, balozi wa kuiwakilisha nchi ughaibuni.

Hiyo ni hatua iliyomvusha Dk. Salim, aliyetumikia huko, pia akajiendeleza kwa elimu ngazi ya juu inayomsaidia utendaji kwenye eneo hilo la sayansi ya siasa na diplomasia kimataifa.

Akiwa katika staili ya kujiendeleza kazini tayari balozi, akatumika na jukumu katika mataifa ya Misri, India, China na Umoja wa Mataifa, jijini New York, Marekani.

Baada ya kutochaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, katika mchuano ambao wasifu wake uliacha mtikisiko na gumzo kwa dunia, baadaye akarejea nchini akitumika katika nafasi ya uwaziri.

Kurejea nchii akadumu kwa miaka kadhaa,Waziri wa Mambo ya Nje, kisha akapanda kuwa Waziri Mkuu kati ya mwaka 1984 na 1985.

Dk. Salim, vilevile ameshika nafasi nyeti na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), kipindi hicho tukasikia simulizi yake kuwezesha kupatikana msaada wa magari mengi ya kutumiwa na jeshi.

Leo naye anaweka historia kuwa Naibu Waziri Mkuu wa kwanza nchini, nafasi ambayo uteuzi wake katika serikali ya awamu ya sita, Dk. Dotto Biteko, sasa ni gumzo.

Marehemu Augustine Mrema naye alishawahi kushika wadhifa huo, Naibu Waziri vilevile.

Miongoni mambo ya kukumbukwa hata inamwongezea heshima maradufu kiuongozi, ni jina lake kutajwa katika watarajiwa wa urais awamu ya pili kwa tiketi ya chama chake CCM.

Kimataifa katika nafasi nyingine, Dk. Salim akajikuta Waafrika wanampendekeza awe Katibu Mkuu wa Umoja wa Afrika, ambako akatumika kwa vipindi vitatu mfululizo, akileta mageuzi makubwa ya utendaji.

Hilo lilikuwa tukio la mwaka 1989, ambako ushuhuda wa ufanisi na uzoefu wake katika dilpomasia kimataifa, akuelekeza katika majukumu yake mapya katika kipya cha kazi jijini Addis Ababa, Ethiopia.

Hapo akawakabirishia tabasamu viongozi wa Afrika na wananchi kwa ujumla, wakishuhudia kwa namna pana ufanisi wenye mahitaji mapya yaliyo na tija na tafsiri pana kuhusu mahitaji ya OAU yanayotumika hadi sasa.

• **Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa zake binafsi na kitabu kinachotarajiwa kuzinduliwa mwezi huu. Simulizi inaendelea Jumatano ijayo.**

---

# WASIRA AMSHTUKIA AKIHISI MUUZA UNGA, JAMBAZI AWEZA KUTINGA IKULU

**INATOKA UK. 11**

ba mpya.

Pambalu anasema kinachoendelea ni kuweka viraka katiba iliyopo, huku matamanio ya Watanzania yakiwa ni kutaka iwepo mpya ambayo wameitolea maoni yao.

"Lengo letu lilikuwa ni kuandika katiba mpya tangu miongo mitatu iliyopita, lakini leo tunaadhimisha miaka 30 ya kushindwa kuiandika , hii ni aibu kwa taifa," anasema Pambalu.

Katibu wa asasi ya Ulingo, Dk. Ave Maria Semakafu, anasema katika miaka 30 ya vyama vingi vya siasa, hakuna uwiano katika uongozi, na kwamba wanawake wanaendelea kubaki katika viti maalum.

Mwanachama wa Chama cha NCCR-Mageuzi, Joseph Selasini, anasema kwa miaka 30 ya demokrasia nchini, rushwa imeshika nafasi kubwa katika uchaguzi na kusababisha wasio na fedha wasichaguliwe.

"Vijana hawapati nafasi za kuwania uongozi kwa sababu hawana pesa za kuhonga, ninadhani Katiba mpya inaweza kuwa suluhisho na changamoto zote zinazojitokeza kwenye uchaguzi," anasema Selasini.

Anafafanua kuwa bila kuwapo katiba mpya, nia nzuri ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kufanikisha malengo yake kwa nchi hayawezi kutimia, na kwamba katiba hiyo inayotokana na maoni ya wananchi ni muhimu.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) Bara, Magdalena Sakaya, anasema kwa miaka 30, hali ya demokrasia nchini imekuwa ikiyumba kwa kutegemea na utawala uliopo.

"Kwa mfano, miaka ya nyuma, upinzani ulikuwa na wabunge na madiwani na wenyeviti wa mitaa wengi, lakini sasa ni wa chama kimoja. Hii imetokana na uongozi uliokuwapo," anasema Magdalena.

Anasema suluhisho la vikwazo hivyo ni kuwapo Katiba mpya inayotokana na wananchi ili iwabane watawala wasipate mwanya wa kuingilia na kuharibu uchaguzi kwa manufaa yao.

Hata hivyo, Wasira anapingana nao na kuwakumbusha kuwa suala la katiba mpya linahitaji utashi wa kisiasa na kwamba kama upinzani usingekimbia Bunge Maalum la Katiba, ingepatikana mapema.





## Mavunde aja na mkakati wa kuongeza ufaulu sekondari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, amekuja na mkakati wa kuongeza ufaulu wa masomo ya sayansi kwa shule za sekondari kwa kuanza kugawa vifaa vya maabara ili kuwawezesha wanafunzi kujifunza ipasavyo.

Mavunde ambaye ni Waziri wa Madini, akizungumza jana kwenye hafla ya kugawa vifaa hivyo, alisema elimu ndiyo mkombozi kwa vijana wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma na amebaini kuwapo na upungufu wa vifaa hivyo kwenye shule za sekondari.

"Baada ya kubaini tuna changamoto katika maabara zetu nyingi za vifaa, nikasema nianze na awamu ya kwanza na hii haitakuwa mwisho nitajitahidi kuzifikia maabara nyingi zaidi. Leo nimeanza na shule tatu na mzigo wa kwanza huu umenigharimu Sh.milioni tisa na nitaendelea kufanya hivi sababu dhamira yangu ni kuhakikisha wanafunzi wetu wanafanya vizuri," alisema.

Alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa mikakati yake ya kukuza elimu katika Mkoa wa Dodoma na hasa Dodoma Mjini.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, John Kayombo, alisema kuwa halmashauri yake imepeleka Sh. milioni 20 kukamilisha ujenzi wa maabara ya Shule ya Sekondari Wella.

Awali, akiongelea mafanikio ya shule hiyo Mkuu wa Shule ya Sekondari Wella, Adelifi Kaizirege, alisema kuwa shule yake imekuwa ikifanikiwa kuongeza ufaulu wa wanafunzi mwaka hadi mwaka.

# Vijana 5,000 kupewa mafunzo ya ujuzi waweze kujiajiri

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imefanya mazungumzo na Benki ya KCB kuhusu utekelezaji wa mradi wa kuwawezesha vijana 5,000 mafunzo ya ujuzi nchini yanayowaandaa kujiajiri na kuajiriwa.

Akizungumza jana jijini hapa katika kuhakikisha malengo ya mradi huo yanafikiwa, Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda, alisema serikali inaunga mkono jitihada za benki hiyo katika kufanikisha vijana wanapata ujuzi.

Alisema wizara ipo tayari kusimamia ubora wa mafunzo na kutoa miongozo stahiki ikiwamo kufanya utafiti ili kuangalia mahitaji na kuongeza ufadhili pale inapowezekana ili kuongeza nguvu zaidi.

Hivyo, aliipongeza Benki ya KCB Tanzania kwa kuja na mradi huo na kusema kuwa una manufaa makubwa kwa taifa kwa kuwa utasaidia vijana kupata mafunzo na hatimaye kuingia kwenye soko la ajira kwa kuajiriwa au kujiajiri.

Naye Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Uhusiano wa KCB, Christine Manyenye kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji, alisema mradi huo unatarajia kuanza mwezi huu na utafanyika katika mikoa sita ya Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro, Shinyanga, Arusha na Kilimanjaro.

Manyenye alisema mradi huu pia utafanyika visiwani Zanzibar (Unguja na Pemba).

"Tunapenda kuishukuru Wizara ya Elimu kwa kulipokea jambo hili ambalo lina manufaa kwa maendeleo ya vijana hapa Tanzania. KCB tunaamini kwamba tukiwapa mafunzo vijana wanaweza kuleta mabadiliko chanya ya kiuchumi kupitia kujiajiri," alisema Manyenye.

Alifafanua kuwa benki hiyo imekuwa ikitekeleza mradi wa Tujiajiri tangu mwaka 2016 na hadi sasa mradi huo umewanufaisha Watanzania zaidi ya 1,579 kwa kuwapa mafunzo ya ufundi stadi na kuwawezesha kuanzisha biashara mbalimbali.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (katikati), akizungumza na viongozi wa Benki ya KCB jijini Dodoma jana. Walijadili kuhusu maeneo ya ushirikiano katika mradi wa kuwawezesha vijana 5,000 kiujuzi nchini unaofadhiliwa na benki hiyo. Kulia ni Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Uhusiano wa benki hiyo, Christine Manyenye na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Carolyne Nombo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanaonunua mifumo kielektroniki nje ya nchi wamchefua Simbachawene

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amezinyooshea kidole taasisi za serikali zinazonunua mifumo kielektroniki nje ya nchi, kuzitaka zishirikiane na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) ili kupata mifumo inayotengeneza ndani ya nchi.

Akizungumza jana jijini hapa baada ya kutembelea Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji Mifumo cha eGA kilichopo Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Simbachawene alisema ni aibu kuona baadhi ya taasisi za serikali zinaendelea kununua mifumo hiyo nje ya nchi badala ya kutumia vijana wa kitanzania kubuni mifumo yao.

"Bado kuna baadhi ya taasisi za serikali ambazo zinanunua mifumo ya kielektroniki kutoka nje wakati hapa nchini taasisi yetu ya eGA inabuni na kujenga mifumo mbalimbali, rai yangu kwao badala ya kuendelea kununua mifumo ambayo inatumia fedha nyingi sana basi waje eGA tusaidiane na wao ili tuweze kujenga mifumo mingi zaidi na vijana mpo hapa mfanyekazi," alisema.

Alisema mifumo ya nje wanatumia fedha nyingi ni bora hizo fedha serikali zitumike kwa shughuli zingine.

"Tuna baadhi ya mifumo tunajivunia inatokana na shughuli za ubunifu na utafiti zilizofanywa na vijana wetu kutoka katika kituo chetu kwa weledi na utaalamu mkubwa, kazi ambazo hapo awali zilikuwa lazima zifanywe na wataalamu kutoka nje ya nchi," alisema.

Kadhalika, alisema wizara kupitia eGA inasimamia na kukiboresha kituo hicho ambacho kimelenga kufanya utafiti kwenye teknolojia mpya zinazoibuka ili Tanzania isibaki nyuma kama Rais Samia Suluhu Hassan alivyoelekeza.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa eGA, Benedict Ndomba, alisema mamlaka hiyo kwa kushirikiana na vyuo vya elimu ya juu, imeandaa programu maalum ya mafunzo kwa vitendo kwenye eneo la TEHAMA ili kuendana na uhalisia kwenye soko na ajira.

Alisema uanzishwaji wa kituo hicho ni moja ya jitihada za serikali kujikita katika kuwa na mazingira ya kufanya utafiti wa kutosha kwenye eneo la TEHAMA.

Alifafanua kuwa mamlaka hiyo inatekeleza programu ya kukuza bunifu kwa wanafunzi wa elimu ya juu, mafunzo ambayo hutolewa kwa vitendo ili wanafunzi wajue na kujifunza nini kinahitajika kwenye sekta.

## RC aagiza mafundi waliopewa kazi zaidi ya moja kupokwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewaagiza viongozi wa halmashauri mkoani hapa kuwanyang'anya kazi mafundi wazembe waliopewa zaidi ya majengo mawili na kuwapa wengine ili kuongeza kasi ya ujenzi.

Alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea miradi ya ujenzi wa nyumba za walimu na sekondari mpya katika Halmashauri za Iramba, Mkalama, Singida DC na Manispaa ya Singida ambapo miradi hiyo inatekelezwa kwa fedha za Mpango wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

"Wahandisi jengo ambalo halina mtu mnamnyang'anya na mnamtafuta fundi mwingine. Haiwezekani fundi akawa na majengo mawili na ndio maana kasi ya ujenzi haiendi haraka kwa sababu baadhi ya mafundi wamepewa zaidi ya majengo mawili," alisema na kuongeza:

"Sasa hakikisheni kila fundi anabaki na jengo moja anayetaka kubaki na majengo mawili aonyeshe uwezo wa kuyamaliza lakini ambaye hawezi anyang'anywe".

Pia aliwaagiza wakuu wa wilaya, wakurugenzi na wahandisi wa wilaya kuhakikisha wanawasimamia kila siku mafundi waliopewa zabuni ya kujenga miradi hiyo na ikabidhiwe kwa muda uliopangwa.

Alisema wakurugenzi na wahandisi wasiwaachie walimu pekee jukumu la kusimamia ujenzi wa miradi hiyo na kwamba wasikubali ujenzi uchelewe kukamilika kwasababu ya uzembe wa fundi.

"Mimi nataka majengo haya yakamilike Septemba 25 mwaka huu, hakikisheni mafundi waliopewa zabuni ya kujenga miradi hii wanaongeza idadi ya vibarua ili kazi iende kwa kasi baada ya muda huo sitahitaji hadithi nyingine," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe, alisema maelekezo waliyopewa watayatekeleza na kwamba ujenzi wa Sekondari ya Utemini ambayo serikali imetoa Sh.milioni 544 unafanyika baada ya wanafunzi kuhamishwa kutokana na majengo yaliyokuwapo kuwa na nyufa.





# Ukosefu miundombinu rafiki kilio walimu wenye ulemavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WALIMU wenye ulemavu mkoani Mbeya wameiomba serikali kuwatatulia kero zinazowakabili ikiwamo ukosefu wa miundombinu rafiki katika sehemu zao za kazi.

Pia wameomba wasaidiwe upatikanaji wa huduma za kijamii kwenye maeneo wanayopangiwa ikiwamo vituo vya kutolea huduma za afya ili wasitumie gharama kubwa kuzitafuta hasa kwa wenye tatizo la ualbino. Walitoa ombi hilo kwenye kongamano la walimu ambalo liliandaliwa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Mkoa wa Mbeya, ambalo liliwahusisha walimu wenye ulemavu kutoka katika wilaya zote za mkoa huo.

Mmoja wa walimu hao, Irene Kessy ambaye ni mwenye ualbino aliomba serikali inapowapangia vituo vya kazi izingatie hali zao kwa maelezo kuwa kwa hali walizonazo wanatakiwa kuwa jirani na vituo vya afya.

Alisema yeye anafundisha Shule ya Msingi Bitimanyanga iliyopo katika Kata ya Kambikatoto wilayani Chunya ambako ni zaidi ya kilomita 200 kwenda katika Hospitali ya Wilaya.

Alisema kutokana na hali hiyo analazimika kutumia gharama kubwa kwenda kuhudhuria kiliniki na hivyo akaiomba serikali kumsaidia asogee karibu na maeneo yenye huduma.

"Lakini naathiriwa na mazingira, mimi nimezaliwa mkoani Kilimanjaro ambako kuna hali ya baridi, sasa nimepelekwa Chunya ambako kuna joto na jua kali ambavyo vinaniathiri ngozi yangu," alisema Irene.

Vilevile alisema maeneo ya vijijini hakuna huduma muhimu kwa wenye ualbino ikiwamo maduka yenye mafuta ambayo wanayatumia.

Naye Mwalimu Tambo Mwakalukwa ambaye ana ulemavu wa miguu alisema shule nyingi hazina miundombinu rafiki kwa walimu wenye ulemavu na hivyo akaiomba serikali kuwasaidia.

Alisema anafundisha Shule ya Sekondari Bujonde iliyopo wilayani Kyela lakini anaishi Kyela Mjini jambo ambalo linamfanya atumie gharama kubwa kwenda na kurudi kazini.

Alisema amenunua gari kwa ajili ya kumsaidia kwenda kazini na kurudi lakini linahitaji matengenezo na hivyo akaiomba serikali imsaidie na kwamba matengenezo hayo yanahitaji Sh. milioni 3.4.

Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Nelusigwe Kajuni, alisema yapo baadhi ya mahitaji ya watu wenye ulemavu yanatolewa na chama na mengine yanatatuliwa na serikali.

Aliyataja mahitaji ambayo yanatolewa na CWT kuwa ni pamoja na fimbo nyeupe kwa walimu wasioona na miwani kwa wenye uoni hafifu.

Alisema mahitaji mengine ikiwamo miundombinu ya shule ni jukumu la mwajiri ambaye ni serikali na hivyo akaahidi kuendelea kufanya mazungumzo na serikali ili iboreshe mazingira.

Mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Robert Mfugale, aliwataka walimu hao wenye ulemavu kuboresha uhusiano kati yao na waajiri, huku akisisitiza kuwa baadhi ya matatizo ya walimu hao yanatatuliwa katika ngazi ya mkoa.



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mbolea ya Yara Tanzania, Winstone Odhiambo, wakifungua kitambaa kuzindua aina saba za lishe mpya ya mifugo, mjini Iringa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni tuhuma kukutwa na meno ya tembo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi mkoani hapa limemkamata mtu mmoja akiwa na vipande viwili vya meno ya tembo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, alimtaja mtu huyo kuwa ni Seleman Ezekia (34) mkazi wa Kijiji cha Imalilo Songwe wilayani Mbarali.

Alisema mtu huyo alikamatwa akiwa amehifadhi meno hayo yenye uzito wa kilogramu 7.5 kwenye mfuko wa sandarusi akiwa kwenye harakati za kutaka kusafirisha kwenda jijini Mbeya.

"Tunaendelea kumhoji mtu huyu na kuendelea kufanya uchunguzi ili baada ya hapo tumfikishe mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria na tunashirikiana na wenzetu wa TANAPA kufuatilia jambo hili," alisema Kamanda Kuzaga.

Aliwataka wananchi wa vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo kushiriki kwenye ulinzi wa maliasili zilizomo ndani ya hifadhi hiyo kwa kutoa taarifa za majangili ili wadhibitiwe kabla ya kutekeleza uhalifu huo. Alisema serikali inatumia gharama kubwa kuwalinda wanyama hao kwa lengo la kuimarisha utalii na kuongeza pato la taifa linalotokana na sekta hiyo.

Hivi karibuni Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na maofisa wa TANAPA waliwakamata pia watu wengine wakiwa na meno ya tembo wakiwa wamejificha kwenye moja ya nyumba za kulala wageni jijini Mbeya.

# Mchungaji ataja mwarobaini mmomonyoko maadili

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MCHUNGAJI wa Kanisa la Waadvetista Wasabato Jimbo la Nyanda za Juu Kusini, Lameck Maligina, amesema mafundisho ya dini pekee ndio yanaweza kusaidia jamii kukabiliana na changamoto ya mmomonyoko wa maadili.

Alitoa rai hiyo kwenye uzinduzi wa kambi ya siku saba ya kanisa hilo, inayofanyika katika Uwanja wa Sabasaba Halmashauri ya Mji wa Njombe.

"Katika mafundisho haya, kuna mafundisho ya maadili mema, mafundisho ya familia, ndoa kwa mgawanyiko mbalimbali na hata watoto, kwa hiyo kwa kuwapo kwao kila mtu kwa rika yake kama ni kijana ambaye hajaoa, ndoa zile changa, ndoa kongwe na watoto wadogo," alisema.

Hata hivyo alisema: "Mafundisho yote ya kila namna yapo ikiwamo ya kimaadili ya kiuchumi, namna ya kujenga maisha kama ni shule kufanya kazi kwa hali zote."

Alisema kupitia kusanyiko hilo wananchi wa Njombe watapona na wale ambao watakuwa tayari kusikiliza sauti ya Yesu.

Katibu Mkuu wa Jimbo, Mchungaji Richard Mashauri kutoka wilayani Kahama mkoani Shinyanga, alisema jamii inapaswa kutafakari kwa kuwa dunia inaisha kwa sababu ya mambo yanayotokea hivi sasa kwenye jamii ni mabaya.

Mmoja wa waumini wa kanisa hilo, Hitro John alisema makambi hayo yanafaida hasa kwa vijana kwa sababu ya masomo mbalimbali yanayotolewa ikiwamo ya uchumi.

## Neema wafugaji, wavuvi bidhaa lishe zikizinduliwa

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

WAFUGAJI na wavuvi nchini wataanza kupata faida kutoka katika mifugo yao baada ya kuzinduliwa kwa bidhaa za lishe bora kwa ajili ya mifugo.

Bidhaa hizo zitatolewa na kampuni ya kutengeneza, kusambaza mbolea ya Yara Tanzania, kwamba zitakwenda kusaidia mamilioni ya wafugaji wa wanyama kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na samaki.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa bidhaa hizo, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, alisema Kampuni ya Yara ni mdau mkubwa wa maendeleo katika sekta ya kilimo nchini.

Alisema inafahamika kwa ubora wa bidhaa zake hususani mbolea mbalimbali za kupandia na kukuzia mazao.

Dendego alisema ubora huo pamoja na maarifa wanayoyatoa kila wakati kwa wakulima umeifanya kampuni hiyo kupendwa na kujikita katika mioyo ya wadau wa hii sekta muhimu.

"Uzinduzi huu wa lishe mpya na bora ya mifugo ni ishara tosha kwamba Yara wanatambua mchango wa wafugaji na wavuvi katika kuboresha maisha ya Watanzania na kuchangia ukuaji wa kipato cha mtu mmoja mmoja na uchumi wa taifa kwa ujumla," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Yara Tanzania, Winstone Odhiambo, alisema: "Tunazalisha bidhaa za lishe bora za wanyama ambazo leo tunazindua kwenye soko la Tanzania. Tunajisikia furaha na tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na serikali, wafugaji na wazalishaji wa chakula cha mifugo ili kuboresha wingi na ubora wa uzalishaji wa maziwa, nyama, mayai na samaki."

Alisema uzinduzi wa bidhaa hiz ni matokeo ya mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula la Afrika (AGRF) uliolenga kuhamasisha nchi za Afrika kuchukua hatua za kuhakikisha usalama wa chakula, kumaliza umaskini na kuliletea bara hili mafanikio.

Mtaalamu wa lishe ya mifugo kutoka Yara, Dk. Peter Mukua, alisema wazalishaji wa maziwa wanahakikishiwa ongezeko la lita tatu zaidi kwa ng'ombe kwa siku kwa kutumia suluhisho ya lishe ya wanyama ya Yara iliyopendekezwa.

Alisema ng'ombe wengi wa asili wa Tanzania ambao kwa sasa wanachangia asilimia 70 ya uzalishaji wa maziwa nchini hutoa kati ya nusu lita na lita mbili za maziwa kwa siku.

Alisema bidhaa hizo zitaongeza kinga ya wanyama na kuboresha uzazi na kumhakikishia mfugaji wa ng'ombe wa maziwa kupata ndama mmoja kila mwaka.





## Serikali yaanza kupima udongo ili kuleta ufanisi katika kilimo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanza kutekeleza mradi wa kupima afya ya udongo ambao umelenga kuleta ufanisi na kuwawezesha wakulima kulima kilimo chenye tija na kupata matokeo mazuri ya uzalishaji.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji Maji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaaema Khamis, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah Ameir, aliyetaka kujuwa lini matokeo ya utafiti wa afya ya udongo yatatolewa na hivyo kutumika kikamilifu na wakulima.

Khamis alisema serikali inatekeleza mradi huo ambao lengo lake kuleta matokeo mazuri ya uzalishaji wa chakula na matunda kutokana na matokeo ya utafiti uliofanywa wa upimaji wa udongo.

Alizitaja hatua zilizochukuliwa kwa sasa ni kuchukuwa sampuli ya udongo na kwenda nayo katika maabara na kupima ili kujuwa aina ya sehemu ya udongo upi mzuri kwa mahitaji ya chakula.

Waziri huyo alisema gari mbili zimenunuliwa na serikali zikiwa na vifaa kwa ajili ya kazi za uchunguzi na upimaji wa udongo ambapo moja tayari limepelekwa katika Kisiwa cha Pemba.

Aidha, alisema kazi ya utafiti imeanza ambapo matokeo yake yanatarajiwa kukamilika na kutangazwa kwa wananchi na wakulima baada ya miezi miwili ijayo.

Akifafanua zaidi kuhusu mradi wa utafiti wa afya ya udongo, Khamis alisema kwa mfano wakulima wa mpunga wanalima kwa kutumia uzoefu tu na matokeo yake uzalishaji wa kilimo hicho umeshuka kwa kiwango kikubwa.

Shamata alisema kwa upande wa kilimo cha mazao ikiwamo muhogo na ndizi, uzalishaji wake umeshuka ikiwamo uvunaji wake na hivyo wakulika kushindwa kulima katika kilimo cha biashara zaidi.

Alisema hivi sasa mahitaji ya soko la muhogo kimataifa ni kubwa ambapo wakulima wanatakiwa kuongeza uzalishaji unaotokana na matokeo ya utafiti wa upimaji wa udongo.

"Soko la muhogo katika nchi za China ni kubwa sana ambapo huu ni wakati muafaka kwa wakulima wetu kulima kilimo zao hilo kitaalamu ili kuweza kupenya katika soko hilo na wakulima kuneemeka," alisema.

# W'biashara wagoma kushusha mizigo Bandari ya Malindi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SIKU chache baada ya serikali kubinafsisha shughuli za uendaji wa Bandari ya Malindi kwa Kampuni ya African Global Logistics (AGL) ya Ufaransa, kumeibuka mgogoro baada ya wafanyabiashara kugoma kuteremsha mizigo yao baada ya kupandishiwa ushuru kwa asilimia 100.

Mgomo huo umetokea juzi ikiwa ni siku ya kwanza kwa kampuni hiyo kutoka Ufaransa kuanza kazi za kusimamia shughuli za uendeshaji ambazo awali zikifanywa na Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC).

Kwa mujibu wa tozo mpya, tani sita za mizigo sasa zinalipwa Sh. 160,000 badala ya Sh. 52,000 kiwango ambacho kilikuwa kinatozwa na ZPC kabla ya ubinafsishaji kufanyika.

Mazao yalioathirika kupitia mgomo huo ni mazao ya viungo, matunda pamoja na mazao ya nafaka yanayoteremshwa kutoka katika Bandari ya Malindi visiwani hapa kwa kutumia usafiri wa majahazi.

"Mazao tunayoleta hayastahamili muda mrefu kukaa bila ya kuoza kama vile nanasi, nyanya, viazi mbatata, karoti, pilipili hoho lakini tunashindwa kutoa mzigo kwa sababu ya ushuru mkubwa tangu bandari kubinafsishwa," alisema Omar Makame mfanyabiashara huyo wakati akizungumza na waandishi wa habari bandarini hapo.

Alisema kimsingi wafanyabiashara hawakatai Bandari kubinafsishwa lakini serikali inapaswa kuwawekea mazingira wezeshi ili kumudu biashara zao bila ya vikwazo vya ushuru.

Alisema athari ya mgogoro huo ni kubwa mbali na kuumiza familia zao kutokana na wao kutofanya biashara pia kutachangia mfumko wa bei wa mahitaji mitaani kwa vile bidhaa za nafaka na matunda na viungo zinaumuhimu mkubwa kwenye sekta ya utalii na kwa wafanyabiashara wadogo Zanzibar.

Sharif Hassan Hamad, mmoja wa mawakala wa mizigo bandarini hapo, alisema hadi sasa anashindwa kutoa mzigo wake kutokana na ushuru mkubwa.

"Kutokana na mabadiliko hayo ya ushuru hatujapewa taarifa na kwa sasa hakuna shughuli yoyote ya utoaji ya upakiaji wa mizigo kwa kutumia majahazi inayofanyika," alisema.

Akizungumzia mgogoro huo, Ofisa Uhusiano wa ZPC, Hassan Amour, alisema viwango hivyo vya ushuru vipo tokea zamani lakini vilikuwa havitumiki ili kuwapa unafuu wafanyabiashara hao.

Hata hivyo alisema baada ya kuingia uongozi mpya wa kampuni ya AGL ya Ufaransa, walihitaji kukabidhiwa kumbukumbu zote za nyaraka za uendeshaji ikiwamo na tozo bandarini hapo na kuanza kuzitumia.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya ZPC, Joseph Meza, akizungumza na waandishi wa habari, alisema kubinafsishwa kwa shughuli za Bandari ya Malindi kutaongeza ufanisi ikiwamo makontena ya mizigo kutolewa kwa muda mwafaka.

Alisema bandari hiyo inakabiliwa na changamoto ya meli kutoshusha makontena kwa wakati na kusababisha tozo za ushuru kuongezeka na kuwabebesha mzigo mkubwa wafanyabiashara na kuwaumiza watumiaji wa mwisho ambao ni wananchi.

Hata hivyo alisema chini ya mkataba wa miaka mitano uliofikiwa, kampuni hiyo itaendesha bandari ya mizigo pekee na huduma za abiria bandari zingine bado zitakua chini ya uongozi wa ZPC.

Alisema hali hiyo inafuatia uamuzi wa serikali kutokana na shughuli za Bandari zinachangamoto nyingi hivyo ili kuimarisha shughuli hizo lazima sekta binafsi na sekta za umma kufanya kazi kwa pamoja.

Aidha, alisema Zanzibar uchumi wake unategemea vitu kutoka nje ya nchi, hivyo ni vyema vitu hivyo vifike kwa haraka na vitolewe bandarini kwa wakati ili kunufaika na teknolojia ambazo nchi za nje zinafanyika.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya AGL, Nicolas Escalin, aliahidi kufanyakazi kwa ufanisi katika uendeshaji wa shughuli ya bandari kwa kushusha mizigo kwa wakati ili kukidhi mahitaji ya wafanyabiashara.

Alisema suala la ushushaji na ucheleweshaji wa mizigo ili kuwa ni changamoto kubwa na kwa sasa watashusha kontena ndani ya siku mbili ambapo awali kontena ikishushwa zaidi ya miezi miwili na kupelekea mfumuko wa bei za bidhaa.



Shehena ya mananasi na bidhaa zingine za nafaka zikiwa kwenye majahazi zikitokea Tanzania Bara, baada ya wafanyabiashara kugoma kuzishusha katika Bandari ya Malindi Unguja jana, kutokana na madai ya kuongezeka kwa ushuru tangu serikali ibinafsishe shughuli za bandari kwa kampuni ya AGL ya Ufaransa. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZAECA yachunguza tukio kiongozi SMZ kutaka kupewa rushwa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) imeanza uchunguzi dhidi ya raia wawili kutoka Uturuki wanaotuhumiwa kutaka kumbambikizia rushwa kiongozi mmoja mwandamizi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (jina halikutajwa).

Uchunguzi huo umeanza kufanyika baada ya kuwasilisha malalamiko yake katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar na ZAECA.

Tukio hilo lilitokea Agosti 28, mwaka huu katika mgahawa wa Rainbow ambao upo katika mji wa kitalii wa Paje Mkoa wa Kusini Unguja. "Ni kweli nimehojiwa mara mbili na ZAECA lakini maelezo yangu tayari nishayatoa kwa mamlaka husika na sioni sababu ya kuzungumza tena," alisema kiongozi huyo.

Taarifa kutoka katika eneo la tukio zimeeleza kuwa raia hao wa kigeni ni Ibrahim Ertan na Deniz Ubety wameingia Zanzibar na kupewa zabuni ya kujenga barabara za ndani kupitia Kampuni ya Aser.

Inadaiwa kuwa raia hao walitaka kuonana na kiongozi huyo lakini walitakiwa waweke miadi na kukutana ofisini kama jambo linahusu shughuli za serikali ili kujadiliwa kwa pamoja na viongozi wa wizara.

Hata hivyo raia hao walipotakiwa kufuata utaratibu, inadaiwa walimtafuta raia mwenzao wa kituruki ambaye yupo Zanzibar kwa miaka mingi akijishughulisha na shughuli za uwekezaji ambaye ndiye mmiliki wa mgahawa huo, Berikhat Aksu na kumwomba kumkutanisha na kiongozi huyo ambaye amekuea na uhusiano wa karibu naye kwa miaka mingi.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa baada ya kiongozi huyo kupigiwa simu na Berikhat Aksu (mmiliki wa mgahawa) na kumwomba kuonana naye, walikubaliana wakutane katika mgahawa huo.

Hata hivyo alipofika (kiongozi) aliwakuta wageni ambao aliwapa ahadi ya kukutana ofisini kwake ili kueleza shida zao jambo ambalo lilimkera na mazungumzo kuvurugika.

"Ni kweli nimehojiwa lakini siwezi kuzungumza chochote zaidi ya yale niliyozungumza ZAECA na sioni sababu ya kuzungumza na nyinyi," Berkhat aliwaambia waandishi wa habari.

Chimbuko la tukio hilo linadaiwa kutokana na ushindani wa kibiashara baada ya kampuni moja kutaka kupewa kazi zote za ujenzi wa barabara za ndani ambazo zinajengwa na kampuni mbili ikiwemo kampuni ya ujenzi ya IRIS na ASER zote kutoka Uturuki.

Hata hivyo raia hao, Ibrahim Ertan na Deniz Ubety hawakuweza kupatikana kuzungumzia tuhuma hizo kupitia simu zao za mkononi kupigiwa mara kadhaa kutopokelewa.

Alipoulizwa kuhusu tuhuma hizo, Mkurugenzi wa ZAECA, Ali Abdallah hakuwa tayari kuzungumzia suala hilo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**JULIETH DAMAS JOSEPH** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index **NO. S1656/0041/2016** kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa kupitia **MOTAMBURU SECONDARY SCHOOL** Mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu. Taarifa polisi: **PHQ/KIL/ROM/1447/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**JULIUS JONAS MBITO** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye usajili namba: **MC 553 DBP.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/URA/14471/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WAISAI MSENYE MAISA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 651 CQB** aina ya Toyota Hiace. Chassis No. **RZH1254008042.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.

Taarifa ya Polisi:

**PHQ/DOD/DOD/RB/1934/2023**

## Tangazo kupotelewa nyaraka ya kiwanja

**Saada Sufian Mbeju** anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba **560 kitalu "HH"** kilichopo Ndala Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Saada kwa simu namba **0754-854339.**

Taarifa ya Polisi:

**PHQ/KIL/MOS/1050/2023.**

Musa Makungu
AFISA ARDHI
MANISPAA YA SHINYANGA
MUNICIPAL LAND OFFICER
SHINYANGA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya..............TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi w a mirathi Na.........................1377/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SEIF MBARAKA JOHARI WA............................**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA**
**NA KURUTHUM SEFU NA IBRAHIM SEFU**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe.............26.................mwezi.........09..........mwaka .....2023............. kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

Imetolewa leo tarehe 12 Mwezi 09 Mwaka 2023

HAKIMU

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI NA. 43 YA MWAKA 2023**

**BAKARI MFAUME KAMBI ..................................................MDAI**

**VERSUS**

**NATIONAL BANK OF COMMERCE ..................................MDAIWA 1**
**MAS & ASSOCIATES CO. LIMITED & COURT BROKER ......MDAIWA 2**

**KWA:**
**NATIONAL BANK OF COMMERCE**
**MAS & ASSOCIATES CO. LIMITED & COURT BROKER**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 21.09. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 15 ya mwezi wa SEPTEMBA, 2023.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

---

**IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.122 Of 2023**

**In the matter of the Estate of the late MAGRETH MPILUGA NHELEKO of Nzuguni B within Dodoma City**

**And**

**In the matter of application for letters of Administration by ANTONY MLEWA KAPUYU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 9, day of 10,2023

Dated at Dodoma this 18 day of September,2023

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......100/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: MINZA JULIUS LUKONU WA MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA KAHABI CHARLES KANZAGA**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 26 Mwezi 09 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia.

**Imetolewa leo tarehe 12 mwezi 09 mwaka 2023**

HAKIMU

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Mackenzie kusotea rumande miezi sita zaidi

**Mombasa, KENYA**

MAHAKAMA Shanzu mjini Mombasa, imeamuru kuendelea kuzuiliwa kwa mshukiwa wa mauaji ya halaiki katika msitu wa Shakahola, Paul Mackenzie (pichani), kwa siku 180 zaidi.

Imesema kwamba, kuzuiliwa kwa mshukiwa huyo ni kwa ajili ya kukamilisha uchunguzi wa kesi inayomkabili yeye na wenzake 29 wanaotuhumiwa kusababisha vifo vya mamia ya watu, kwa kuwashauri wajizuwie kula na kunywa, hadi kufa.

Takriban watu 429 waliripotiwa kufariki kutokana na kutii amri hiyo na miili yao ilifukiliwa kutoka kwenye Msitu wa Shakahola katika Kaunti ya Kilifi.

Upande wa mashtaka uliiambia mahakama hiyo kwamba haukuwa umekusanya ushahidi wa kutosha.

Kulingana na upande wa mashtaka, miili 360 kati ya iliyofukuliwa ilikuwa imeoza sana.

Hatua za kufukua makaburi, zimesitishwa kwa sasa, lilikuwa likifanyika kwa awamu. Shauri hilo litasikilizwa Oktoba 12, mwaka huu.

**DW**



# Asilimia 50 ya kuku, nguruwe hupewa ARVs

**Kamapla, UGANDA**

MAMLAKA ya Taifa ya Udhibiti wa Dawa Uganda (NDA), imekiri kwamba ilijua dawa za kupunguza makali ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), zilitumika kunenepesha mifugo ikiwamo kuku na nguruwe lakini haikutoa onyo kwa jamii.

Inspekta Mkuu wa mamlaka hiyo, Amos Atumanya, aliliambia bunge hivi karibuni kwamba walikuwa wanajua dawa hizo za kukabiliana na VVU zilikuwa zikipatiwa nguruwe na kuku ili kuwatibu mwaka 2014, ingawa haikuonya umma.

Atumanya alisema ilikuwa hatari kwa binadamu kutumia kiwango kidogo cha dawa hizo katika chakula.

Msemaji huyo alisema iwapo kuna hatari yoyote ya kiafya, ingeonya umma huku kazi ya mamlaka hiyo ikiwa kudhibiti matumizi ya dawa na sio chakula wala chakula cha wanyama.

Ripoti ya hivi karibuni kutoka Chuo Kikuu Makerere, iligundua zaidi ya theluthi moja ya kuku na asilimia 50 ya nguruwe, waliofanyiwa vipimo walikuwa na chembechembe za dawa hizo za kukabiliana na ugonjwa wa Ukimwi.

Nyama hiyo ilinunuliwa kutoka masoko yalioko mjini Kampala pamoja na mji wa kaskazini wa Lira.

Mbele ya Kamati ya Bunge kuhusu Ugonjwa wa Ukimwi, Atumanya alisema NDA ilifanya uchunguzi mwaka 2014 kuhusu matumizi ya dawa za kukabiliana na Ukimwi katika kilimo cha wanyama.

"Hivyo basi tulikuwa tukijaribu kutafuta njia nyingine ya kukabiliana na hali hiyo," alisema.

Mhojiwa mmoja wa utafiti huo wa Chuo cha Sayansi ya Afya katika Chuo Kikuu cha Makerere, alisema nguruwe ambao walipewa dawa za kupunguza makali ya VVU hukua haraka na kunenepa na huuzwa haraka.

Atumanya alisema jambo hilo linaweza kusababisha matatizo makubwa kwa binadamu waliokula nyama hiyo na kuambukizwa VVU.

"Kuna uwezekano ugonjwa kuwa sugu dhidi ya dawa za ARVs. Katika siku zijazo ikiwa unazihitaji, basi utakuta ARVs hizi hazifanyi kazi kwa baadhi ya watu."

Takriban watu milioni 1.4 nchini, wanaishi na VVU/UKIMWI, kulingana na Umoja wa Mataifa (UN).

Ripoti ya NDA mwaka 2014, iligundua kuwa dawa za kupunguza makali ya VVU zilitumika zaidi kutibu homa ya nguruwe Afrika, ambayo pia inajulikana kama Ebola ya Nguruwe na kwa sasa haina tiba.

Pia ilithibitisha madai kwamba ARVs zilikuwa zikitumika kutibu ugonjwa wa Newcastle katika kuku. Msemaji wa NDA alitetea uamuzi wake wa kutotangaza matokeo yake.

Aliongeza kwamba mdhibiti huyo alianzisha hatua kadhaa za kukomesha matumizi mabaya ya dawa za kulevya, jambo ambalo lilisababisha watu kadhaa kukamatwa na kufunguliwa mashtaka.

**BBC**

# Waandamana wakidai mafuriko ya kizembe

**Derna, LIBYA**

MAMIA ya wakazi wa mji wa Derna mashariki mwa Libya, waliandamana dhidi ya viongozi wa eneo hilo, zaidi ya wiki moja baada ya mafuriko makubwa yaliyoua maelfu ya watu katika mji huo.

Nyumba ya Meya wa Mji wa Derna, Abdulmenam al-Ghaithi. Bw Ghaithi, imeteketezwa pamoja na maofisa wengine wa manispaa ya Derna, kusimamishwa kazi na Waziri Mkuu wa Mashariki mwa Libya, Osama Hammad.

Waandamanaji hao walimkosoa kiongozi wa Bunge la Mashariki mwa Libya, Aguila Saleh na mamlaka za mitaa, walilaumu kwa mafuriko ambayo yamesababisha vifo vya karibu watu 4,000, kulingana na takwimu zilizotolewa na Umoja wa Mataifa (UN).

Katika taarifa ya pamoja, waandamanaji hao walisema wanataka uchunguzi wa haraka kuhusu maafa hayo na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya viongozi waliohusika.

Pia walidai fidia, uchunguzi juu ya fedha za jiji na ujenzi wa Derna. Mashariki mwa Libya inatawaliwa na serikali nyingine, tofauti na serikali inayotambuliwa na UN yenye makao makuu katika mji mkuu wa Libya, Tripoli.

Wataalamu kadhaa na mashirika ya kibinadamu, wamependekeza kuwa mafuriko yangeweza kuzuiwa ikiwa mamlaka za mitaa, ziliwahamisha wakazi au angalau kutoa onyo kuhusu kimbunga Daniel.

Wataalamu pia walisema kutelekezwa kwa mabwawa ya jiji hilo na mamlaka, kulisababisha kubomoka kwa mabwawa hayo yaliyosababisha mafuriko.

**BBC**

**Waandamanaji hao walimkosoa kiongozi wa Bunge la Mashariki mwa Libya, Aguila Saleh na mamlaka za mitaa, walilaumu kwa mafuriko ambayo yamesababisha vifo vya karibu watu 4,000, kulingana na takwimu zilizotolewa na Umoja wa Mataifa (UN).**

# TWIGA STARS YAPAA IVORY COAST NA MATUMAINI KUFUZU WAFCON

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Taifa ya Soka ya Wanawake, Twiga Stars, imeondoka jijini Dar es Salaam jana kuelekea Ivory Coast kwa ajili ya mechi ya kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wanawake dhidi ya nchi hiyo, itakaochezwa Ijumaa mjini Yamoussoukro.

Twiga itakuwa na kazi moja tu ya kusaka tiketi ya kucheza michuano hiyo kama kaka zao, Taifa Stars iliyofuzu fainali za WAFCON zitakazofanyika nchini Ivory Coast Januari mwakani.

Fainali za WAFCON nazo zinatarajiwa kuchezwa mwakani nchini Morocco katika tarehe itakayopangwa baadaye.

**Kocha Kuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, amesema wameridhishwa na maandalizi yaliyofanyika na ana imani wachezaji wake watakitafsiri kile alichokifundisha mazoezini kukiweka uwanjani ingawa haifahamu vema timu ya Ivory Coast inavyocheza.**

"Matayarisho yetu yamekwenda vizuri, tumekuwa na takriban siku 10 za maandalizi kujiandaa na mchezo huu, ni mchezo muhimu kwetu kwa maana ni wa kufuzu fainali za Afrika kwa wanawake, matamanio yetu ni kufanya vizuri na kusonga mbele.

Matayarisho yetu yamelenga zaidi mahitaji jinsi ya kucheza mechi ya kwanza ugenini na ile ya pili hapa nyumbani, tumewaelekeza wachezaji wetu na nadhani wameyashika na nikitazama morali yao iko juu, naamini kabisa watayatafsiri vizuri yale ambayo tumeyafundisha kwenye mazoezi yetu," alisema Shime.

Hata hivyo, alikuwa na wasiwasi kidogo kwa sababu haitambui vema timu anayokwenda kucheza nayo, hivyo mechi ya kwanza ugenini alisema itabidi wacheze kwa tahadhari.

"Tulishindwa kufuzu WAFCON iliyopita, lakini tumeangalia tulipojikwaa, nadhani yale tuliyoyapitia hatuwezi kuyapitia tena kwa sasa ingawa hatujui sana uwezo wa wapinzani wetu kwa hiyo inatupa kazi ngumu kidogo sisi watu wa benchi la ufundi kutengeneza mbinu za kuweza kuwakabili, ila tutahakikisha tunacheza kwa uangalifu mechi ya kwanza ili yasijirudie yale ya msimu uliopita tulipopoteza dhidi ya Namibia tukashindwa kufuzu," alisema.

## 'NCBA Gofu Series 2023' kupigwa J'mosi

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya mchezo wa Gofu ya 'NCBA Golf Series 2023' yamepangwa kufanyika Jumamosi ijayo kwenye viwanja vya Dar es Salaam Gymkhana na yatashirikisha wachezaji wa mchezo huo kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania.

Wachezaji watakaoshiriki watasaka nafasi ya kwenda kushiriki fainali za mashindano hayo kwa upande wa Afrika Mashariki yatakayofanyika Nairobi, Kenya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Benki ya NCBA, washindi wa tatu wa juu watawakilisha nchi kwenye fainali hizo za Afrika Mashariki.

"Safari ya mashindano haya mwaka huu imepita katika nchi za Kenya, Uganda, Rwanda na sasa Tanzania kisha fainali ya mwisho itafanyika Nairobi, Kenya kuwapata washindi wa jumla wa mashindano hayo makubwa," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kinachofanya mashindano hayo kuwa ya kipekee zaidi ni nafasi yanayowapatia washindi mbali na zawadi lakini kwenda kushiriki fainali za Afrika Mashariki nchini Kenya.

"Kutakuwa na makundi matatu ya mabingwa, mshindi wa jumla, mshindi wa jumla kwa wanaume, na mshindi wa jumla kwa wanawake. Safari ya mabingwa hawa haitaishia kwenye viwanja vya Gymkhana Club badala yake watasafiri kwenda Nairobi, Kenya kuungana na mabingwa wengine kwa ajili ya kuwapata mabingwa wa jumla wa 'NCBA Golf Series' 2023.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa mabingwa wa mwaka huu watagharamiwa kila kitu na Benki ya NCBA kwenda Nairobi kushiriki fainali hizo za mwisho.

Katika mashindano hayo ya Nairobi, mshindi kutoka katika kila kundi atapata zawadi ya Sh.100,000 za Kenya (sawa na Sh. 1,703,042 za Tanzania).

**UZINDUZI...**




Meneja wa Chapa ya Safari Lager, Pamela Kikuli, akipiga mpira kuashiria uzinduzi wa mashindano makubwa ya mpira wa miguu yajulikanayo kama Safari Lager Cup, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Kocha wa mashindano hayo, Sekilojo Chambua na Jamhuri Kihwelo 'Julio'. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Timu Ligi Kuu kulamba mil. 44/- mechi 1 Safari Lager Cup*

**Na Mwandishi Wetu**

BIA ya Safari Lager imezindua mashindano makubwa ya mpira wa miguu yajulikanayo kama Safari Cup yenye lengo la kuibua vipaji katika mikoa mbalimbali nchini ambapo wataunda timu itakayojulikana kama Safari Champions – mabingwa wapya katika mpira (The New Order of Champions).

Mashindano hayo yamezinduliwa jana katika viwanja vya Leaders Club, Dar es Salaam ambapo wadau mbalimbali wa soka walihudhuria hafla hiyo ya uzinduzi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Meneja wa Chapa ya Safari Lager, Pamela Kikuli, alisema Bia ya Safari, ambayo ni ya mabingwa, imeamua kuja na kampeni hii ili kuibua vipaji vipya kabisa vya mpira wa miguu kwani wanaamini kuna vipaji vingi nchini ambavyo havijaibuliwa.

Alisema mashindano hayo yatafanyika katika mikoa minne - Mbeya (FFU Polisi) Oktoba 7, Arusha (Uwanja wa Ngarenaro) Oktoba 21, Mwanza (Uwanja wa Nyamagana) Novemba 4 na Dar es Salaam (Viwanja vya Kinesi) Novemba 18, mwaka huu.

Pamela alisema vijana wenye umri wa miaka 18 na zaidi wataitwa kwenye usaili ili washiriki katika mashindano ya mtoano yatakayofanyika ili kuchagua vijana ambao watawakilisha timu ya kila mkoa kati ya mikoa minne iliyochaguliwa.

"Baada ya hapo timu zile za mkoa zitatumika kuchagua vijana ambao watAunda timu moja kubwa ya wachezaji 22 ambao watacheza mechi ya kirafiki na timu mojawapo ya Ligi Kuu ambayo itatangazwa hapo baadaye. Vile vile mchezaji mmoja atapata fursa ya kuchaguliwa na mawakala wa Ligi Kuu Bara ili kuwezeshwa kuchezea timu kubwa hapo baadaye.

"Mawakala hawa watakuwa wakifuatilia vipaji vya wachezaji wa Safari Lager Cup Champions ili kuendeleza vipaji vyao katika soka," alisema Pamela.

Alisema kama motisha, timu hii ya Safari Champions itakayochaguliwa kucheza mechi ya kirafiki na timu mojawapo ya Ligi Kuu, itajinyakulia kitita cha Sh. milioni 44 na itajulikana kama Timu ya Mabingwa ya Safari Cup yaani Safari Cup Champions.

"Wakati wa mashindano hayo, tungependa kuwaalika mawakala wa klabu mbalimbali za Ligi Kuu waje kuangalia baadhi ya wachezaji ambao wanaweza kujiunga na timu kubwa za Ligi Kuu," alisema.

Wakati wa uzinduzi huo, makocha Jamhuri Kihwelo, 'Julio' mmoja wa makocha bora Tanzania na aliyewahi pia kuichezea Klabu ya Simba na Timu ya Taifa (Taifa Stars) na Sekilojo Chambua, aliyewahi kuichezea Tukuyu Stars ya Mbeya na Yanga, walishiriki katika mdahalo wa aina yake ambao uliratibiwa na mtangazaji maarufu wa Clouds Fm na mhamasishaji wa masuala ya mpira wa miguu, Mbwiga Mbwiguke.

## ZISIKUPITE

### CHELSEA, BAYERN KWA AARON

KLABU za Chelsea na Bayern Munich zinamfuatilia Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 25, baada ya mlinda mlango huyo wa England na Arsenal kuachwa nje katika mechi ya 'Washikabunduki' hao dhidi ya Everton Jumapili. ***(Daily Mail)***

### GNABRY ATAKIWA UNITED

MANCHESTER United inaandaa ofa ya kumnunua mshambuliaji wa Bayern Munich na Ujerumani, Serge Gnabry, huku klabu hiyo ikiwa tayari kutoa takriban pauni milioni 52 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Fichajes)***

### GIMENEZ JICHO OLD TRAFFORD

MLINZI wa Atletico Madrid na Uruguay, Jose Maria Gimenez mwenye umri wa miaka 28, pia anavutiwa na Manchester United. ***(FourFourTwo)***

### ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inafikiria kutoa ofa ya pauni milioni 52 kumnunua kiungo wa West Ham, Lucas Paqueta. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alihusishwa na Manchester City msimu wa majira ya joto, lakini uhamisho huo ulitibuka kufuatia uchunguzi wa madai ya ukiukaji wa kamari uliofanywa na Mbrazil huyo. ***(Daily Mail)***

### DIAZ KWENDA QATAR

MCHEZAJI wa Liverpool, Fabricio Diaz mwenye umri wa miaka 20, anawaniwa na Klabu ya Al Gharafa ya nchini Qatar huku kiungo huyo wa Uruguay pia akizivutiwa na Brighton na Barcelona. ***(Fabrizio Romano)***

### DRAXLER AJIFUNGA AL AHLI

KIUNGO wa kati wa Ujerumani, Julian Draxler mwenye umri wa miaka 29, amejiunga na Klabu ya Al Ahli SC ya Qatar kutoka Paris St-Germain kwa mkataba wa kudumu. ***(Fabrizio Romano)***

### TRENT KUFUNGWA

MLINZI wa England, Trent Alexander-Arnold, anakaribia kujifunga upya Liverpool kwa kutia saini mkataba mpya licha ya Barcelona na Real Madrid kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(90min)***

### SILVA BEI JUU CITY

KIUNGO wa Manchester City na Ureno, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 29, atagharimu klabu yake inayofuata pauni milioni 50 kutokana na mkataba wake mpya ikiwa ni pamoja na kipengele cha kuuzwa. ***(Fabrizio Romano)***

### BIANCONE ATUA OLYMPIACOS

MLINZI wa Ufaransa, Giulian Biancone mwenye umri wa miaka 23, amekamilisha uhamisho wa kudumu kutoka Nottingham Forest kwenda Olympiacos. ***(The Athletic)***

### GILCHRIS AONGEZA MKATABA

MLINZI wa Chelsea mwenye umri wa miaka 19, Alfie Gilchrist ameongeza mkataba wake wa mwaka mmoja hadi Juni 2025. ***(Standard)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: NI RAHISI KWETU KUBEBA LIGI YA MABINGWA

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City itakuwa na "urahisi" zaidi wa kutetea taji lao la Ligi ya Mabingwa Ulaya kuliko ilivyokuwa mwanzo wakati wakipambana kwa muda mrefu kushinda shindano hilo kubwa kwa klabu barani Ulaya, amesema Pep Guardiola.

**City walinyanyua taji lao la kwanza la Ligi ya Mabingwa kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Inter Milan mjini Istanbul Juni, na hivyo kumaliza miaka mingi ya kukaribia kulitwaa.**

Alipoulizwa kuhusu nafasi ya City ya kutetea taji hilo kabla ya mechi yao ya kwanza ya Kundi G nyumbani dhidi ya Red Star Belgrade,

**Kigumu zaidi kushinda ni cha kwanza, ni muhimu wachezaji wasijisikie wametulia...**

Guardiola aliwaambia waandishi: "Itakuwa rahisi zaidi. Kigumu zaidi kushinda ni cha kwanza."

Hata hivyo, Guardiola alisema wachezaji wake hawapaswi kujisikia raha na kuongeza: "Kesho (jana) ni hatua ya kwanza. Tutajaribu kupata pointi tatu za kwanza.

"Ni muhimu wachezaji wasijisikie wametulia. Kwa klabu yetu kushinda Ligi ya Mabingwa ni jambo la ajabu, lakini kwa mtazamo ni klabu ngapi zimeshinda?

"Hatujafanya chochote maalum na moja tu, lakini tunajivunia sana."

Guardiola alisema majeruhi watatu Jack Grealish, John Stones na Mateo Kovacic, ambao wote walikosekana katika ushindi wa mabao 3-1 wa City dhidi ya West Ham United Jumamosi, bado hawajapona.

"Nadhani wanazidi kuwa bora," aliongeza Guardiola.

"Natumaini wanaweza kuwa dhidi ya Nottingham Forest kwenye Ligi Kuu Jumamosi au mechi zijazo.

"Angalia jinsi tunavyojidhihirisha bila wao katika michezo iliyopita. Tunatumaini watarejea hivi karibuni kwa sababu tunahitaji ushindani."

HABARI MICHEZO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,154,8

MECHI KALI
YOUNG AFRICANS
VERSUS
NAMUNGO
1 | 1.11
X | 5.25
2 | 13.11

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Jackline Mosha - 0652 277 XXX
2. Hassan Shekighenda - 0654 355 XXX
3. Anthony Manji - 0655 434 XXX
4. William Mwanjela - 0656 307 XXX
5. Felix Mwanjejele - 0672 611 XXX
6. Mussa Kaduma - 0672 848 XXX
7. Emanuel Seje - 0673 672 XXX
8. Kombo Athuman - 0676 256 XXX
9. Emanuel Wami - 0678 200 XXX
10. Hadija Boto - 0717 594 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MAN UNITED MAJANGA JUU YA MAJANGA



**MANCHESTER,** England


BEKI wa Manchester United, Aaron Wan-Bissaka, atakuwa nje ya uwanja kwa muda baada ya kupata jeraha wakati wakipoteza kwa mabao 3-1 nyumbani dhidi ya Brighton wikendi iliyopita, klabu hiyo ya Ligi England imetangaza.

United iliongeza kuwa suala hilo bado linatathminiwa, lakini beki huyo wa kulia anaweza kuwa nje ya uwanja kwa "wiki kadhaa."

Kwa mujibu wa ripoti ya gazeti la The Athletic, mchezaji huyo wa Kimataifa wa England, atakuwa nje ya uwanja kwa miezi miwili kutokana na jeraha la misuli ya paja.

Tatizo la Wan-Bissaka linaongeza orodha inayoongezeka ya majeruhi hapo United, huku kiungo Mason Mount na mabeki Luke Shaw na Raphaël Varane pia wakiwa nje kwa wiki za hivi karibuni.

United itasafiri kwenda kwa Bayern Munich katika mchezo wao wa kwanza wa Kundi A wa Ligi ya Mabingwa Ulaya leo Jumatano, kabla ya kucheza na Burnley kwenye Ligi Kuu Jumamosi.



# *James hana mpango wa kuondoka Chelsea*

**LONDON,** England

REECE James ataendelea kujitolea kikamilifu kwa Chelsea na havutiwi na ofa kutoka mahali pengine, kwa mujibu wa 90min.

Ripoti kutoka Hispania zimedokeza Real Madrid inataka kumnunua beki huyo wa kulia wa 'The Blues' msimu ujao wa majira ya joto, huku wengine wakienda mbali na kudai kuwa James yuko tayari kuhamia Santiago Bernabeu.

Wakati Madrid wanania ya kumnunua James, 90mi inaelewa kuwa nahodha huyo wa Chelsea hana nia ya kuondoka pale Stamford Bridge.

James, ambaye alitia saini mkataba mpya wa miaka sita mwaka jana, amezungumza waziwazi kuhusu nia yake ya kufanikiwa akiwa na Chelsea na analenga kuwaongoza The Blues hao kurejea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England baada ya mwaka wa misukosuko chini ya umiliki mpya.

Kwa mujibu wa 90min James amesisitiza kuwa amejitolea kikamilifu kwa Chelsea.

Licha ya Madrid, James alishawahi kuwindwa Barcelona, huku Bay Munich na bosi wa zan Thomas Tuchel wan hamika kuwa masha wakubwa wa mche huyo mwenye umri miaka 23, lakini ku doka Chelsea ni jan lisilowezekana kama ili

James amevun mwanzo mgumu wa k peni ya sasa, akiug jeraha la msuli wa paja tika mchezo wa ufun wa msimu ambalo lim weka nje tangu wa huo na kumpa mche mpya Malo Gusto nafas kuanza.

## HABARI MICHEZO


361,566/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/09/23 | 17:00 | Middlesbrough FC vs Southampton FC | 2.65 | 3.35 | 2.47 |
| 02. 23/09/23 | 17:00 | Dundee FC vs Kilmarnock FC | 2.50 | 3.20 | 2.70 |
| 03. 23/09/23 | 17:00 | Airdrieonians FC vs Raith Rovers FC | 2.43 | 3.20 | 2.55 |
| 04. 23/09/23 | 17:15 | CA Osasuna vs Sevilla FC | 2.50 | 3.20 | 2.70 |
| 05. 23/09/23 | 19:30 | Burgos CF vs Elche CF | 2.80 | 3.00 | 2.60 |
| 06. 23/09/23 | 19:30 | Werder Bremen vs FC Cologne | 2.55 | 3.50 | 2.50 |
| 07. 23/09/23 | 19:45 | NEC Nijmegen vs FC Utrecht | 2.55 | 3.55 | 2.47 |
| 08. 23/09/23 | 20:00 | Casa Pia Lisbon vs Vitoria SC Guimaraes | 2.55 | 3.05 | 2.80 |
| 09. 23/09/23 | 22:00 | Stade Brest 29 vs Olympique Lyon | 2.55 | 3.50 | 2.50 |
| 10. 24/09/23 | 14:00 | FC Metz vs Strasbourg Alsace | 2.85 | 3.20 | 2.42 |
| 11. 24/09/23 | 15:30 | Ajax Amsterdam vs Feyenoord Rotterdam | 2.48 | 3.60 | 2.50 |
| 12. 24/09/23 | 17:00 | Cercle Brugge vs Union Saint-Gilloise | 2.65 | 3.40 | 2.45 |
| 13. 24/09/23 | 17:15 | Real Oviedo vs Real Valladolid | 2.75 | 2.85 | 2.70 |
| 14. 24/09/23 | 17:15 | Rayo Vallecano vs Villarreal CF | 2.55 | 3.40 | 2.55 |
| 15. 24/09/23 | 18:05 | Montpellier HSC vs Stade Rennes | 2.65 | 3.45 | 2.43 |
| 16. 24/09/23 | 21:45 | Torino FC vs AS Roma | 2.85 | 2.95 | 2.55 |
| 17. 24/09/23 | 22:00 | Atletico Madrid vs Real Madrid | 2.65 | 3.35 | 2.47 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 20/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 1061 | Ural Yekaterinburg vs Lokomotiv Moscow | 2.34 | 3.31 | 2.70 |
| 15:00 | 2621 | CSKA Moscow vs Sochi | 1.69 | 3.60 | 4.37 |
| 16:00 | 2950 | AL Ain vs AL Safa (Sa) | 1.69 | 3.42 | 4.43 |
| 16:00 | 5828 | El Daklyeh vs Enppi Club | 2.54 | 2.99 | 2.79 |
| 16:30 | 3804 | TJ Medzibrod vs Rimavska Sobota | 3.80 | 4.00 | 1.64 |
| 17:00 | 2810 | ND Dravinja vs Tabor Sezana | 1.78 | 3.63 | 3.68 |
| 17:00 | 3882 | NK Bistrica vs NK Fuzinar Ravne | 1.46 | 4.15 | 5.47 |
| 17:00 | 5659 | NK Ilirija vs ND Gorica | 3.01 | 3.22 | 2.14 |
| 17:15 | 1518 | Malavan Bandar Anzali vs Peykan FC | 2.16 | 2.70 | 3.76 |
| 17:15 | 4491 | Rubin Kazan vs Rostov | 2.23 | 3.26 | 2.90 |
| 17:15 | 5814 | Akhmat Grozny vs Zenit St Petersburg | 3.17 | 3.42 | 2.03 |
| 17:30 | 3515 | Lille vs Olimpija Ljubljana | 1.22 | 5.98 | 10.97 |
| 18:00 | 4718 | Havadar vs Teraktor Sazi | 3.20 | 2.80 | 2.23 |
| 18:20 | 1736 | AL Adalh vs AL Qaisoma | 1.69 | 3.30 | 4.40 |
| 19:00 | 1976 | Young Africans vs Namungo | 1.11 | 5.25 | 13.11 |
| 19:15 | 2465 | KA Akureyri vs Keflavik IF | 1.54 | 4.19 | 4.70 |
| 19:30 | 1133 | Albinoleffe vs Pro Patria | 2.13 | 3.13 | 3.55 |
| 19:30 | 1934 | Sassari Torres vs Carrarese | 2.48 | 3.14 | 2.88 |
| 19:30 | 2533 | Pro Vercelli vs AC Pro Sesto | 2.06 | 3.24 | 3.61 |
| 19:30 | 3871 | Arzignanochiampo vs Alessandria | 2.28 | 3.15 | 3.20 |
| 19:30 | 4137 | AC Lumezzane vs Fiorenzuola | 2.43 | 3.14 | 2.93 |
| 19:30 | 5966 | Trento Calcio 1921 vs Legnago | 2.01 | 3.30 | 3.72 |
| 19:45 | 3931 | Galatasaray vs Copenhagen | 1.56 | 4.02 | 5.05 |
| 19:45 | 4748 | Real Madrid vs Union Berlin | 1.40 | 4.35 | 6.85 |
| 20:00 | 5119 | SV Donaustauf vs DJK Ammerthal | 3.25 | 3.65 | 1.85 |
| 20:30 | 1167 | SuperSport Utd vs Kaizer Chiefs | 1.90 | 3.02 | 4.31 |
| 20:30 | 1230 | Orlando Pirates vs Mamelodi Sundowns | 2.78 | 2.93 | 2.57 |
| 20:30 | 5193 | TS Galaxy FC vs Cape Town City | 2.39 | 2.88 | 3.08 |
| 20:30 | 5912 | BSV Rehden vs Atlas Delmenhorst | 2.42 | 3.41 | 2.54 |
| 21:30 | 1252 | Club Almagro vs San Martin SJ | 2.51 | 2.80 | 2.90 |
| 21:45 | 1463 | Hull City vs Leeds | 3.66 | 3.41 | 1.91 |
| 21:45 | 1489 | Watford vs West Bromwich | 2.15 | 3.23 | 3.18 |
| 21:45 | 2055 | Blackburn vs Sunderland | 2.20 | 3.50 | 2.86 |
| 21:45 | 2316 | Huddersfield vs Stoke City | 2.78 | 3.17 | 2.41 |
| 21:45 | 3254 | Millwall vs Rotherham | 1.69 | 3.53 | 4.67 |
| 21:45 | 3363 | Renate vs Atalanta BC U23 | 2.04 | 3.25 | 3.67 |
| 21:45 | 3669 | Giana Erminio vs Mantova | 3.30 | 3.20 | 2.20 |
| 21:45 | 3747 | Vecomp Verona vs Vicenza | 2.43 | 3.04 | 3.04 |
| 21:45 | 5159 | Padova vs Novara | 2.07 | 3.29 | 3.55 |
| 22:00 | 1099 | Barracas Central vs Banfield | 2.38 | 2.84 | 3.04 |
| 22:00 | 1309 | Sporting Braga vs Napoli | 3.81 | 3.52 | 1.84 |
| 22:00 | 1878 | Sevilla FC vs Lens | 1.84 | 3.47 | 3.86 |
| 22:00 | 3202 | Bayern Munchen vs Manchester Utd | 1.56 | 4.17 | 4.75 |
| 22:00 | 3333 | Norwich City vs Leicester | 2.57 | 3.41 | 2.45 |
| 22:00 | 3542 | Benfica vs RB Salzburg | 1.39 | 4.57 | 6.56 |
| 22:00 | 4006 | Defensa Justicia vs CA Tigre | 2.35 | 3.05 | 2.89 |
| 22:00 | 4162 | Arsenal vs PSV Eindhoven | 1.41 | 4.53 | 6.28 |
| 22:00 | 4480 | Real Sociedad vs Inter | 2.85 | 3.09 | 2.40 |
| 22:15 | 5763 | Vikingur Reykjavik vs KR Reykjavik | 1.52 | 4.28 | 4.79 |
| 23:15 | 5275 | CS Union Huaral vs Los Chankas CYC | 2.97 | 3.38 | 2.10 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# KOCHA ALIYEIPASUA FUTURE FC SHIRIKISHO ATIMKA SINGIDA FG

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Singida Fountain Gate FC, Mjerumani Ernst Middendorp, hatokuwa sehemu ya benchi la ufundi la timu hiyo katika michezo yao ijayo ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC kesho na ule wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Future FC ya Misri.

Kocha huyo ambaye hana zaidi ya wiki mbili tangu ajiunge na Singida FG kuchukua nafasi Mserbia Hans van Pluijm, katika mechi yake ya kwanza akiwa na timu hiyo ya mkoani Singida, aliiongoza kushinda bao 1-0 kwenye mechi ya kwanza ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Saalam mwishoni mwa wiki.

Middendorp aliondoka jana kurejea kwao baada ya kutokuwa na maelewano mazuri na menejimenti ya timu hiyo na nafasi yake kwa sasa inashikiliwa na Mkurugenzi wa Ufundi, Ramadhani Nsanzwirimo akisaidiana na Mathias Lule, aliyekuwa kocha msaidizi ambaye hakuwapo kwenye mechi iliyopita dhidi ya Future FC, lakini sasa amerejeshwa.

**Nipashe juzi ilihudhuria katika mazoezi ya timu hiyo ambapo Kocha Middendorp hakuwa sehemu ya benchi la ufundi huku kikosi kikisimamiwa na Nsanzwirimo na Lule.**

Kwa mujibu wa chanzo chetu cha habari cha kuaminika ndani ya Singida FG, Middendorp hakufurahishwa na kuingiliwa na majukumu yake jambo ambalo lilimfanya kuchukua uamuzi huo wa kuomba kuondoka.

"Menejimenti ya timu walifanya kikao juzi na Kocha Middendorp ambaye hakuridhishwa na kile ambacho alidai kuingiliwa katika majukumu yake na ameondoka na kurejea kwao," kilieleza chanzo chetu.

Aidha, Nipashe lilimtafuta Mtendaji Mkuu wa Singida Fountain Gate FC, Olebile Sikwane, ambaye alikiri kuondoka kwa Middendorp na kurejea kwao kwa sababu ya kutokuwa na maelewano mazuri na uongozi.

Alisema kwa sasa wakati timu iko kwenye maandalizi ya mechi mbili ya Ligi Kuu dhidi ya Azam FC na Shirikisho dhidi ya Future FC, wanakwenda kutafakari yapi yaliyojiri kwenye kikao.

"Tunaheshimu mkataba wake, tumempa muda wa kutafakari kwa sasa timu itakuwa chini ya mkurugenzi wa ufundi akisaidiwa na wasaidizi waliopo Lule na Thambo Senong atakuwa na timu kwa kipindi chote, hadi hapo kocha huyo atakaporejea.

"Tunaimani baada ya kutafakari atarejea katika kikosi kwa sababu tunaheshimu mkataba wake ambao tuliingia naye hivi karibuni wa kukinoa kikosi cha timu yetu," alisema Sikwane.

Aliongeza kuwa kuondoka kwa kocha huyo hakutaathiri timu yao kuelekea maandalizi ya mechi zilizopo mbele yao kwa sababu wanaimani na walikuwapo kuendelea na programu ambayo Middendorp ameiacha.

## Robertinho bado yupo

INATOKA UK. 24

chake kwa ajili ya kufikia malengo yao ikiwamo kushinda kila mechi.

Katika hatua nyingine Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally, alisema bado wanaimani na Kocha Robertinho kuwafikisha katika malengo wanayoyatarajia.

Alisema wanaridhishwa na matokeo wanayoyata uwanjani, lakini bado hawajafikia ile Simba wanayoitaka, na kwamba hakuna ukweli juu ya tetesi zilizopo kuwa kocha huyo amepewa mechi tatu.

"Tunaimani na benchi la ufundi kutufikisha kwenye nchi ya ahadi, tunaridhishwa na kupata matokeo mazuri, lakini bado hatujafikia kuona ile Simba biriani.

"Kwa sasa tunaelekea kwenye soka ambalo tunalitarajia kuliona kwa sababu ya wachezaji wapya kutengeneza muunganiko na wale wa msimu uliopita," alisema Ahmed.




Beki wa Yanga, Ibrahim Bacca, akiwa mazoezini, timu hiyo itashuka Uwanja wa Azam Complex, Chamazi leo kuvaana na Namungo FC kwenye mechi ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu Bara. **PICHA: YANGA**

## *Yanga yarejea kwenye shoo*

INATOKA UKURASA 24

kwenye ubora gani, tumefika wapi," alisema kocha huyo ambaye msimu uliopita alikuwa Kocha Msaidizi wa Yanga chini ya Nasreddine Nabi ambaye kwa sasa naye ametimkia FAR Rabat ya Morocco.

Kuhusu afya za wachezaji wake, alisema mshambuliaji Reliant Lusajo, tayari amepona na ameanza mazoezi isipokuwa Partene Counou ambaye hatakuwapo katika mchezo wa leo.

Mwakilishi wa wachezaji wa Namungo, Jacob Masawe, alisema wamejipanga vizuri kukutana na Yanga na kwamba watatumia mbinu walizopewa na mwalimu wao kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

Michezo

Jumatano Septemba 20, 2023

Nipashe



Majanga juu ya majanga Man Utd UKURASA 22

# Yanga yarejea kwenye shoo zake za 5G Ligi Kuu Bara

## ●●● Gamondi apagawa na utayari wa wachezaji, Namungo nao wasema wapo...

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

MABINGWA wa Tanzania Bara, Yanga, leo wanarejea kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kucheza dhidi ya Namungo FC katika mechi itakayopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

**Yanga inarejea kwenye Ligi Kuu tangu Agosti 29, mwaka huu ilipocheza dhidi ya JKT Tanzania kwenye uwanja huo huo ikishinda mabao 5-0.**

Itakuwa ni mechi ya raudi ya tatu kwa timu hizo, huku Yanga ikiwa imeshinda mechi mbili za mwanzo mabao 5-0, dhidi ya KMC na JKT Tanzania.

Kwa upande wa Namungo inakwenda kuivaa Yanga ikiwa haijashinda mechi yoyote ile, ikichapwa bao 1-0 nyumbani Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa Lindi dhidi ya JKT Tanzania na sare ya bao 1-1 mechi ya pili dhidi ya KMC.

Kocha Mkuu wa Yanga Muargentina Miguel Gamondi amesema mpaka sasa hajaamua nani ampange na nani ampumzishe kwenye kikosi hicho kwa sababu ana wachezaji ambao kila mmoja anaweza kucheza mechi za Ligi Kuu.

"Kikosi changu nitakipanga kesho baada ya kuangalia vitu vingi, tulianza maandalizi ya mechi hii baada ya mechi dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan nchini Rwanda na tangu jana (juzi) tulikuwa tunafanyia kazi ya kuangalia jinsi gani tutaicheza mechi hii, tulikuwa tunaangalia utimamu wa mwili wa baadhi ya wachezaji pamoja na majeraha, tunataka kupata matokeo mazuri na mchezo mzuri kwenye mechi hili," alisema kocha huyo.

Alisema katika kikosi chake anataka kumpa nafasi kila mmoja na wachezaji wake wengi wanaweza kabisa kucheza mechi za Ligi Kuu, lakini hata hivyo pia inategemea anapambana na mpinzani gani.

"Kila mchezaji anayekuwa kwenye benchi katika kikosi changu anaweza kuanza na kucheza mechi ya ligi, kila mara natakiwa kuwapumzisha wachezaji kwa ajili ya kuwawekea akiba ya utimamu wa mwili na kutokuwa wachovu wanapokuwa uwanjani, lakini hiyo yote inategemea na mpinzani tunayekwenda kucheza naye, ni kweli nataka kumpa nafasi kila mmoja acheze, lakini wakati mwingine ukubwa wa michuano na uhitaji wa matokeo unabana kutokuwapo kwa kitu hicho, ila tutajaribu hilo kesho," alisema.

Kwa upande wa mwakilishi wa wachezaji wa Yanga, Crispin Ngushi, alisema: "Tumejipanga vema kuhakikisha tunapata alama tatu katika mchezo wetu wa kesho (leo), ambao utakuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa."

Kocha Mkuu wa Namungo, Mrundi Cedric Kaze, alikiri kuwa anakwenda kucheza mechi na timu ambayo iko kwenye kiwango cha juu kwa sasa.

"Tumejiandaa vizuri, tumepata muda wa kutosha kufanya maandalizi, ukiangalia mechi ya mwisho tulipocheza dhidi ya KMC mpaka sasa unakaribia mwezi mzima, tunakwenda kucheza na timu ambayo kwa sasa ipo kwenye kiwango bora kabisa, hata hivyo itakuwa mechi nzuri kwetu kujua tupo

INAENDELEA UKURASA 23



Robertinho

# Robertinho bado yupo sana Simba, aanika mkakati

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikiwa kwenye maandalizi ya mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Coastal Union, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Robertinho Oliveira, amekuja na mbinu mpya ya kimkakati kwa ajili ya mechi yao ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos ya Zambia huku uongozi ukisema bado wanaimani naye.

Simba ambayo imetoka kupata sare ya mabao 2-2 nchini Zambia dhidi ya Power Dynamos, inatarajia kushuka dimbani keshokutwa kuwakaribisha Coastal Union mchezo wa Ligi Kuu Tanzania utakaopigwa Uwanja wa Uhuru na kutumia mchezo huo kufanyia kazi programu yake mpya.

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho alisema ameona mapungufu ya kikosi chake katika kipindi cha kwanza na kufurahishwa na waliocheza kipindi cha pili, hivyo anataingia na mbinu mpya katika mchezo dhidi ya Coastal Union.

Alisema mbinu hiyo ataanza kuifanyia kazi katika mchezo dhidi ya Coastal Union ikiwa ni kipimo cha maandalizi ya mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos.

"Tumerejea nyumbani kuendelea na programu ya maandalizi ya mechi yetu ijayo, nitakuja na mbinu mpya ambayo nitaanza kuifanyia kazi dhidi ya Coastal Union kwa ajili ya maandalizi yetu ya mechi ijayo ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Nimefurahishwa na kipindi cha pili walivyocheza ukiangalia Fabrice Ngoma, Luis Miquissone, Jean Baleke na Saido Ntibazonkiza walicheza vizuri mechi iliyopita, lakini ni muda wa kufanyia kazi changamoto zilizojitokeza Zambia," alisema Robertinho.

Alisisitiza kuwa anaamini wachezaji wake wote wanauwiano mzuri na atahakikisha anaendelea kuimarisha kikosi

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >